# Yehova-Yire #1

Grass Valley, California, Amerika
Julai 05, 1962

1 Hebu tubakie tukiwa tumesimama kwa kitambo kidogo tunapoinamisha vichwa vyetu kwa ajili ya neno la maombi. Tunapoinamisha vichwa vyetu, katika maombi, ukiwa na kitu fulani kwenye moyo wako unachotaka Mungu afanye kwa ajili yako, inueni tu mikono yenu. Bwana atujalie haya mahitaji sasa tunapoinamisha vichwa vyetu na mioyo yetu mbele Zake.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunakiendea Kiti Chako cha Enzi cha Rehema tena, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana mkuu wa Mungu. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya nafasi ya kuja pamoja na uhakika kuwa Wewe utasikia na kujibu kile tunachoomba. Tunaomba, Baba, kuwa utatusamehe dhambi zetu, yaani, kutokuamini kwetu. Na, Baba, tunaomba kuwa utatupa sisi imani, wingi wa imani jioni hii. Na Wewe unajua nini kilichokuwa nyuma ya kila mkono pale, chini katika moyo. Wao walihitaji kitu fulani, Bwana. Wao waliinua mkono wao kwa unyenyekevu, wakitarajia kitu fulani kutoka Kwako. Na mimi naomba, Baba wa Mbinguni, chochote kile, kuwa utawajalia hicho watu Wako.

Tunakushukuru kwa ajili ya ule ujio jioni iliyopita. Tunaomba kuwa utaturudia jioni hii pamoja na wingi wa nguvu na neema, na utatujalia shauku za moyo wetu, kwani, kwa kweli shauku yetu ni kufanya Mapenzi Yako na kuona Mapenzi Yako yakifanyika. Nasi tunajua Mapenzi Yako ni nini kuhusu wagonjwa, kuwa Wewe ulipigwa mgongoni Mwako kwa ajili ya uponyaji wetu, "Kwa kupigwa Kwake sisi tulipona." Na, Baba, tunaomba kuwa-kuwa Mapenzi Yako makuu yatafanyika jioni hii, ili kutupa sisi imani ya kuamini hilo, kwa wingi, kuwa kila mtu mgonjwa aweze kuponywa, na kila mtu aliyepotea aweze kukumbuka kuwa Yeye alichubuliwa kwa ajili ya maovu yetu. Tujalie hilo, Bwana.

Hebu wao wajue kwamba maadam kuna-Dhabihu iliyotapakaa damu Pale kwa ajili yao, dhambi zao haziwezi kuonekana na Mungu. Lakini kama wao watakufa pasipo kuungama Hiyo hadharani na kuikubali Hiyo, na kuzaliwa mara ya pili, hapatakuweko na njia hata kidogo ya wao kuweza kuingia katika ule Ufalme. Na hii iwe jioni ambayo kila mtu toka chini ya Damu ataingia kwa haraka chini ya Damu jioni hii, katika Jina la Bwana Yesu. Na sisi tutakupa Wewe sifa. Amina.

3 Ni tunu kuu mno kuwa hapa jioni hii na kunena tena. Na jana jioni tulikuwa na wakati wa ajabu, ujio wa Bwana. Lakini niliwaweka mno. Kamwe siwezi kumaliza huduma katika wakati uliopangwa, kwa namna fulani.

Ni kama vile kuna jua zaidi kidogo leo hii. Mimi nilikuwa…Mwanangu mdogo, Joseph, alinifuata kwenda kuogelea. Hivyo pale mahali tunakokaa palikuwa na kisima kidogo, kilichowekewa uzio nyuma pale, na yeye akasema, "Njoo, nitazame, baba. Mimi naweza kuogelea."

Mimi nikasema, "Vema."

Mimi nikaenda chini pale asubuhi hii, nikachukua Biblia yangu, na baadhi…ili kuandika muhtasari fulani. Na nilipokuwa nikisoma kwa kupekua kwa undani, yeye…huyu anakuja hapa akiwa amevaa nguo zake ndogo za kuogelea, yeye akasema, "Nitazame mimi, baba, naweza kupiga mbizi!" Vema, kama niliwahi kumwona chura akirukia ndani ya maji! Na yeye akaibuka, na maji yakiwa yanatoka kwenye pua zake na kinywani, yeye akasema, "Je, nilifanya namna gani?"

Mimi nikasema, "Unafanya vizuri."

4 Na mimi nikawaza juu ya wakati mmoja nilipomwambia kitu kile kile baba yangu. Kidimbwi kidogo cha zamani, kabla hatujaenda mtoni, kulikuweko na kidimbwi, na sisi watoto ilikuwa ni shida kuondoa utando wa kijani kwenye hicho, na sisi tunge- … maji hayakufikia hata kina cha inchi sita. Na mimi niliendelea tu kumwambia baba yangu, "Mimi naweza kuogelea."

Hivyo Jumapili moja alasiri yeye akatoka nje pale. Nao walikuwa na kiboksi kidogo cha sabuni kilichokuwa kimekaa pale. Nami nikarudi vichakani na kuvua nguo zangu, kile kilichokuweko cha kuvua; kuvuta tu upande mmoja, unajua. Na ni wangapi waliowahi kuona kimoja kama hicho? Sawa. Nikiwa nimevaa tu jozi ya ovaroli, isiyokuwa

na vining'inizo; majani makavu ya mifugo yaliyosokotwa pale, kwa ajili ya mikanda ya kushikilia suruali, na ndipo msumari tu. Unavuta tu msumari na, ni hilo tu unalopaswa kufanya, unarukia moja kwa moja ndani. Na kupigapiga ndani ya hayo, na tope likiruka takriban juu kiasi hicho. Baba yangu akiwa ameketi pale, akiwa ananitazama. Mimi nikasema, "Mimi ninafanyaje?"

Akasema, "Toka huko na uende kuoga!" Mimi nilikuwa ninawaza hilo limechukua muda mrefu kiasi gani!

5 Na, unajua, muda huwa unatuacha tu, sivyo? Inaonekana kama kwamba hatuna tu wakati, tena, wa kufanya mambo. Na wakati haumngoji mtu yeyote. Hivyo ni lazima tufanye kazi wakati tunapoweza, kwa sababu saa inakuja wakati hiki kizazi kitaondoka, na kitakuweko kizazi kingine kinachokuja, kama kuna kizazi kingine. Kwa kweli, mimi nasema hilo kwa moyo wangu wote, (Mimi sijui Yeye anakuja lini; hakuna mmoja wetu anayejua), lakini, kwa kweli, mimi siamini kutakuweko na kizazi kingine. Mimi naamini Kristo atakuja katika kizazi hiki. Mimi sijui ni wakati gani, sasa, huenda ikawa jioni hii, au huenda ni miaka kumi tokea sasa, au ishirini, lakini mimi naamini Yeye atakuwa katika kizazi hiki. Mimi ninaamini hilo. Kama Yeye hatakuja, mimi nataka niishi tu kama Yeye alivyokuwa, kwa vyovyote, kwa sababu mimi najua kuwa hiyo huenda ikawa siku yangu ya mwisho, au siku yako ya mwisho.

6 Na ndipo, kumbukeni, kama sisi tukiondoka kabla ya Yeye kuja, tutakuwa juu na katika Uwepo Wake, au, tufufuliwe kabla ya hao wengine hawajabadilishwa. "Baragumu ya Bwana italia, hao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Ndipo sisi tulio hai na tuliobakia tutabadilishwa katika kitambo kidogo, kufumba na kufumbua, na kuchukuliwa juu pamoja nao, ili kukutana na Bwana hewani." Tazama huo mpango wa ufufuo. Unaona, Mungu anajua kuwa tunatamani kukutana na wapendwa wetu. Na kama tutafika pale tukutane na Yeye kwanza, tutakuwa tunatazama huku na huku ili kuona kama mama au baba na hao wengine walikuwa pale. Lakini mnaona jinsi, Roho Mtakatifu katika hekima Yake? "Neema ya Ajabu," hiyo ni-hiyo ni wakati kutakuweko na wakati wa kuabudu. Mnafikiri natenda kimzaha sasa, nitafute mimi juu Pale! Unakwenda kuwa wakati wa ajabu kwangu mimi na sisi sote tutakapofika Pale.

7 Sasa hebu tusome baadhi kutoka kwenye Biblia ya zamani iliyobarikiwa hapa jioni hii. Hebu tufungue pale kwenye Warumi, sura ya 4, na tusome tu sehemu kutoka kwenye Kitabu cha Warumi. Nataka kusoma sehemu mbili. Sasa katika Kitabu cha Warumi, sura ya 4, aya ya 17.

> *(Kama ilivyoandikwa, Nimekuweka kuwa baba wa mataifa mengi,) mbele zake yeye aliyemwamini, yaani Mungu, mwenye kuwahuisha wafu, ayatajaye yale yasiyokuwako kama kwamba yamekuwako.*
>
> *Naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili aweze kuwa baba wa mataifa mengi; kama ilivyonenwa, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.*
>
> *Yeye asiyekuwa dhaifu wa imani, alifikiri hali ya mwili wake uliokuwa umekwisha kufa, akiwa amekwishakupata umri wa kama miaka mia, wala … hali ya kufa ya tumbo lake Sara.*
>
> *Lakini akiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu kwa imani, akimtukuza Mungu;*
>
> *Huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi.*
>
> *Walakini haikuandikwa kwa ajili yake tu kwamba ilihesabiwa kwake;*
>
> *Bali na kwa ajili yetu sisi mtakaohesabiwa vivyo hivyo, sisi tunaomwamini yeye aliyemfufua Yesu Bwana wetu katika wafu;*
>
> *Ambaye alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili mpate kuhesabiwa haki.*

8 Ee, nalipenda Hilo iliyoje! Hilo ni mojawapo ya kusoma kwangu Andiko nilipendalo la Biblia, kwa sababu Hilo ni chanya mno kile Mungu alichokuwa, kile Yeye alichoahidi na kuapa kuwa Yeye angelifanya. Na sasa mimi nilichagua hili somo kwa sababu kwamba mimi nafikiri hilo juu ya mkutano wowote, kuona imani ile tuliyoona ikifanywa hapa jioni iliyopita, kuwa hakuna mtu aliye mnyonge miongoni mwetu bali kile kilichoponywa. Zile nguvu za Mungu zilizokuja na kile Yeye alichofanya! Ndipo mimi nikawaza, kama tungeweza kujenga hapa jambo fulani lililo chanya, tukipata mafanikio kwenye lengo,

basi lingekuwa zuri mno kiasi gani wakati tungeweza kugonga ile jioni kuu au saa ya kilele.

9 Na ni lazima sisi tukumbuke kuwa hakuna chochote kinachoweza kufanyika pasipo imani, na hicho inapasa kiungamwe kwanza. Kwani Yeye ni-Yeye ni Mwanzilishi wa imani, tunajua hilo, na kwamba hakuna chochote kinachoweza kufanyika pasipo imani. Na pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu.

Na sasa Yeye ni Kuhani Mkuu wa ungamo letu. Sasa ile-ile King James hapa, katika Kitabu cha Waebrania, inaweka hilo "ukiri." Kukiri na kuungama ni kitu kile kile, kukiri na kuungama. Kuungama humaanisha "kusema kitu kile kile"; "Kwa kupigwa Kwake sisi tulipona," unaona, "Sasa kwa Uzima Wake mimi nimeokolewa." Na sasa basi, kwanza, inatupasa sisi tukiri hilo; na Yeye huketi kama Mpatanishi, na Mpatanishi pekee kati ya Mungu na mwanadamu, na Yeye anaketi pale ili kuomba juu ya kile tunachokiri kuwa Yeye amefanya. Ni kitu muhimu na kikuu iliyoje!

10 Na sasa nataka kusoma Andiko lingine, linalopatikana katika Kitabu chacha Mwanzo, sura ya 22, na hebu tuanze kusoma hapa takriban aya ya 7.

> *Isaka akasema na Abrahamu baba yake, akisema, Babangu! Naye akasema, Mimi hapa, mwanangu. Akasema, Tazama! Moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa?*
>
> *Abrahamu akasema, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka mwanangu. Basi wakaendelea wote wawili pamoja.*
>
> *Wakafika mahali pale alipoambiwa na Mungu, Abrahamu akajenga madhabahu huko, akaziweka tayari kuni, kisha akamfunga Isaka mwanawe, akamweka juu ya-juu ya madhabahu, juu ya zile kuni.*
>
> *Abrahamu akanyosha mkono wake, akakitwaa kisu ili amchinje mwanawe.*
>
> *Ndipo malaika wa BWANA akamwita kutoka mbinguni, akaema, Abrahamu! Abrahamu! Naye akasema, Mimi hapa.*
>
> *Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno, kwa maana sasa ninajua ya kuwa-ya kuwa unamcha Mungu, na nimeona wewe…hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee.*
>
> *Abrahamu akainua macho yake…akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa penye pembe zake katika kichaka. Basi Abrahamu akaenda akamtwaa…awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe.*
>
> *Abrahamu akapaita mahali hapo Yehova-yire, kama watu wasemavyo hata leo, Katika mlima wa BWANA itapatikana.*

11 Kile ninachotaka kupata somo pale, kama lingeitwa somo, "*Yehova-Yire*." Hilo neno humaanisha "Bwana atajipatia Mwenyewe dhabihu." Kama Yeye hana yoyote, Yeye anaweza kujipatia moja. Nina shukurani mno kwa ajili ya hilo. Sasa hili somo kuu! Na sasa kwa kusoma pale, kuwa "Abrahamu hakuyumba kwenye ile ahadi kwa kutokuamini; lakini alikuwa imara, akimtukuza Mungu."

Sasa, Abrahamu alikuwa ndiye ambaye Mungu alimfanyia agano na ahadi; na Abrahamu, siyo yeye pekee, bali Uzao wake baada ya yeye, "Abrahamu na Uzao wake." Na sasa kumbukeni hili sasa. Kama sisi tukiwa tumekufa katika Kristo, sisi ni Uzao wa Abrahamu kama tumezaliwa upya. Sasa, hebu tuwe waangalifu hasa juu ya hili sasa tunapojifunza hili somo. Na sasa kama utasikiliza kwa makini, mimi nina hakika Roho Mtakatifu atakufunulia. Utashika tumaini, na ndipo hilo litaangaza hili jiji lionekane na kila kitu kilichokuzunguka, kama tu tukitumia muda wa kutosha na kulidaka hilo wazo, kile Roho Mtakatifu anachojaribu kutupa sisi. Sasa, Abrahamu, aliitwa, yeye ndiye aliyepewa ile ahadi, kwa Abrahamu na Uzao wake.

12 Sasa kuna mengi mno leo hii, marafiki, yanayoitwa Ukristo, ambao siyo Ukristo.

Sasa, mimi nachukia tu kusema hili. Lakini ni bora mimi nisimame hapa na kuwa maarufu hasa miongoni mwa watu, na-na kila mtu akikupigapiga mgongoni mwako kukupongeza, na kila kitu namna hiyo. Lakini basi inanipasa kukutana na hilo kundi kwenye Hukumu, ili kutoa hesabu kwa ajili ya hilo. Hivyo mimi-mimi inanipasa tu niwe mwaminifu.

Sasa tunaweza kutazama makusanyiko, na ulimwengu leo hii, kile kinachoitwa Ukristo, na tukute kwamba ni maili milioni mbali na Ukristo. Na imebashiriwa katika Biblia kuwa itakuwa hivyo. Sasa wengi humkubali Kristo katika njia ya kusema, "Vema, mimi namwamini Yeye." Mbona, yule Mwovu huamini vivyo hivyo. Unaona? Na wengi wao hujaribu kulipokea hilo juu ya msisimko, wanasema, "Vema, mimi nilinena kwa lugha. Nilicheza katika Roho." Mimi nimewaona wachawi wakifanya kitu kile kile, na wachezaji wa kipepo katika Afrika; hakika, wakinena kwa lugha, na kunywa damu kutoka kwenye fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kumwita yule Mwovu. Mama yangu ni Mhindi, chotara wa Kihindi, na-na watu wake. Mimi nimewaona hao wakichukua penseli na kuiweka chini namna hiyo, na kuitazama hiyo penseli ikitembea na kuandika katika lugha isiyojulikana, wao wakiwa wamesimama pale na kufasiri hiyo, wakimwita yule Mwovu. Hakika.

13 Unaona, huwezi kuenenda kwa misisimko. Unaona, maisha yako unayoyaishi yanashuhudia kile wewe ulicho. Unaona? Haidhuru ni msisimko wa aina gani, huwezi kuweka msingi wa Ukristo kwenye msisimko.

Ni maisha! Yesu alisema, "Kwa tunda lao utawajua." Siyo kwa kukiri kwao, siyo kwa kile wao wanachosema. Na Yesu pia alisema, "Mnanisogelea kwa midomo yenu, lakini moyo wenu uko mbali na Mimi." Huko ni, huko ni kukiri kwao. Unaona, maisha yako yanasema hicho. Na kama mtu anasema kuwa yeye anamwamini Mungu, na kulikana Neno moja la hii Biblia, au analibadilisha Hilo kwa njia yoyote, mbona inapasa hilo liwe kosa.

14 Unasema, "Hilo halileti tofauti yoyote juu ya haya mambo madogomadogo." Hakika linaleta tofauti.

Neno moja dogo ndilo lililotuingiza sisi katika shida yote hii; siyo kutokuliamini Hilo, bali kuliweka tu Hilo mahali pasipo Pake. Hawa alifanywa tu na Shetani akose Hilo, alimpa tu Hawa hoja. Kule chini kwa Ndugu Williams, tulijifunza haya yote nilipokuwa kule chini katika Santa Maria. Hicho ndicho kitu kilichotuleta sisi kutoka Bustani ya Edeni, na kusababisha kila mtoto mgonjwa. Kama, mimi nilivyoomba kwa ajili ya mtoto mdogo mwenye kifafa akiwa amelala pale, kitambo kidogo kilichopita, nikiwa ninaingia ndani. Nini kilichosababisha hilo? Kwa sababu Hawa kamwe hakuacha kuliamini Hilo, lakini yeye alihoji tu, kwamba hili lingelikuwa la busara hili lingekuwa sahihi. Na hilo lilisababisha kila kifo, kila ugonjwa, kila huzuni, kila maumivu ya moyo. Na tunakwendaje kurejea ndani? Kama hilo lilisababisha-kama hilo lilisababisha miaka elfu sita ya hili, tunarejea vipi tukiwa na chochote kilicho pungufu ya kila Neno kamilifu kama ambavyo Hilo limeandikwa?

15 Yule Mwovu alishinda vita juu ya jamii ya mwanadamu kwa kuhojiana kiakili pamoja na jamii ya mwanadamu. Kwa kutoa tu hoja, "Mbona, inabakia tu kuhoji, je, hili litakuwa? Imebainika kuwa." Kama hoja zenyewe ni kinyume na Neno, basi kutoa hoja ni kosa! Lile Neno ndilo sahihi, kama tu ambavyo Hilo limeandikwa! Usiweke fasiri yoyote ya binafsi. Liseme tu Hilo jinsi Hilo lilivyoandikwa, na uliamini Hilo namna hiyo. Unaona? Mungu amelituma Hilo. Hilo liko tu kabisa jinsi linavyopaswa kuwa, hivyo hebu tuliamini tu Hilo namna hiyo.

Sasa, ni Neno, kila Neno! Kila … Roho Mtakatifu ndani ya mtu; kila sentensi ya Biblia, Roho Mtakatifu ndani yako ataitikia kwa "amini," kwa sababu Roho Mtakatifu aliiandika Biblia. Na kama Yeye yuko ndani yako, Yeye anawezaje kusema, "Vema, Hilo lilikuwa kwa ajili ya kipindi kingine, Hilo lilikuwa kwa ajili ya *hiki*, au Hilo lilikuwa kwa ajili ya *kile*"? Yeye anawezaje kusema hilo na awe Roho Mtakatifu ndani yako? Hawezi kufanya hilo. Inampasa Yeye asema "amina" kwa Hilo!

16 Sasa, kama mimi nilivyosema siku ile nyingine, kitu cha kwanza Mungu alichowapa watu Wake, ili kujiwekea nacho ngome, kilikuwa Neno. Na kamwe Yeye hajabadilika. Yeye hawezi kubadilika. Sasa, kanuni za imani haziwezi kutenda kazi, madhehebu hayawezi kufanya kazi, elimu hawezi kufanya kazi, hakuna chochote cha hivi vitu, kila kimoja kimeshindwa kabisa na kitashindwa. Kuna Kitu kimoja pekee kitakachofanya kazi, hicho ni Neno.

Na njia moja pekee tunayoweza kuja kwa Neno, ni kwa njia ya Damu. Mahali pekee ambapo mtu aliwahi kumwabudu Mungu, inapasa aje chini ya Damu. Hakuna maandalizi mengine hata kidogo. Huwezi kuja chini ya jina la Methodisti, huwezi kuja chini ya jina la Pentekoste, huwezi kuja chini ya jina la Katoliki. Kuna dazeni ya makanisa ya Katoliki,

tofauti, tofauti na lingine, la Orthodox, la Kiyunani, na la Kirumi, na yamegawanyika vibaya kama Protestanti. Waprotestanti, Methodisti, Baptisti, Presibiteri, Lutheran, Katoliki, ee, kila, yote ni aina mbalimbali. Na ndiyo hayo hapo, unaona. Lakini kuna msingi mmoja kwa ajili ya ushirika, huo ni chini ya Damu! Na hiyo Damu ni Uzima, na huo utakubaliana siku zote na Neno, siku zote pamoja na Neno.

17 Sasa, tunajua uzima uko katika jinsia ya kiume, uko katika damu, hemoglobini. Kupitia pale kuku anaweza kutaga yai, lakini kama yeye hajawa na ndege wa kiume, kamwe halitaanguliwa. Hakika, halijarutubishwa. Hivyo ndivyo nilivyo na, nimefanya matamshi makali, nikisema ndege wa kike anaweza kuatamia kiota kilichojaa mayai, na yeye anaweza kuwa mwaminifu kwa hayo atakavyo kuwa, yeye anaweza kukaa juu yake, pamoja na mabawa yake, na kuyageuza kila baada ya dakika chache ili wawe na uhakika ya kuanguliwa. Na-na yeye atapata njaa mno, na kufunga, awapo juu ya kiota, ili kuwa mwaminifu kwa hayo mayai, hadi anadhoofika mno asiweze hata kuruka kutoka kwenye kiota. Kama yeye hakuwa na ndege wa kiume, na hayo mayai yawe yamerutubishwa, yatakaa hapo hapo katika kiota na kuoza kama yeye hakukutana na mwenzi. Hilo ndilo hasa.

Na hivyo ndivyo takriban makanisa yetu yamefikia, yanawapokea tu ndani kundi fulani la waumini, wakikiri ungamo la kawaida la baridi, dansi fulani ya kimafumbo au msisimko fulani. Na wao wanafanya nini? Kutokuamini Neno, hadi tunacho tu kiota kilichojaa mayai yaliyooza. Ni wakati wa kusafisha kiota na kuanza upya. Hadi wao waje wakutane na Yule wa Kiume, Kristo Yesu, na kupata kuzaliwa mara ya pili kwa Neno. Ndipo wanaanguliwa, kwa sababu ni Uzima.

18 Wakati fulani uliopita nilikuwa ninakula chakula cha usiku pamoja namhubiri wa zamani wa Methodisti, na nikasikia redioni Saa ya Kilimo kutokea-kutokea Louisville, Chama cha 4-H walikuwa wanaongea, kwamba "Wao walikuwa na mtambo ambao uliweza kuzalisha mbegu ya mhindi kama tu ambavyo zinakua shambani." Wakasema, "Huo ungetengeneza aina ile ile ya chembechembe za mahindi, aina ile ile ya mkate wa mahindi, ilikuwa ni mhindi ule ule. Wanaikata hiyo namna ile, wanaiweka chini ya mwanga, wanaipeleka maabara; moyo wake uko katika mahali sahihi, na kila kitu, na kiasi kile kile cha unyevu, kalsiumu, potashi, chochote kile kilichoko katika mhindi kimekaa tu sawasawa." Wakasema, "Kama ungelichukua kiasi kidogo kutoka kwenye gunia la ile iliyolimwa shambani, na lile gunia la ile iliyotengenezwa kwa mtambo, au iliyotengenezwa, na kuyachanganya, kamwe hungeweza kuonyesha tofauti kwa macho yako ya kawaida, au kwa kuitenganisha ziwe mbalimbali, au sayansi yoyote isingeweza kuona tofauti yoyote. Njia pekee ungeweza kuona tofauti ilikuwa ni kuziotesha hizo." Hilo linadhihirisha.

19 Mtu anaweza kuonekana kama Mkristo, yeye anaweza kutenda kama Mkristo, yeye anaweza kumwigiza Mkristo. Lakini isipokuwa yeye awe na mbegu ya Uzima ndani pale, yeye hawezi kufufuka tena; inapasa awe na mbegu ya Uzima ndani pale, awe na Uzima wa Milele.

Na mtu yeyote aliyejifunza Kiyunani, anajua kuwa "Milele" hutoka kwenye neno Zoe, ambalo humaanisha "Uzima wa Mungu Mwenyewe," ambao unafanyika kuwa sehemu Yake; kama ambavyo wewe ni sehemu ya baba yako. Wewe unafanyika kuwa sehemu ya Mungu. Na Uzima wa Mungu Mwenyewe, unagawanywa na kuwekwa ndani yako, na Huo hauwezi kufa, kwa sababu Huo ni wa Milele. Kila kitu kinachokuwa na mwanzo, kina mwisho; lakini Yeye kamwe hakuwahi kuwa na mwanzo, hivyo Yeye hawezi kuwa na mwisho. Yeye ni wa Milele, na wewe ni wa Milele pamoja na Yeye. Huwezi kufa tena kama ambavyo Yeye hawezi kufa, kwa sababu wewe unafanyika kuwa sehemu yake. Wewe umezaliwa na Yeye. Amina. Naendelea tu kuzungumza juu ya hilo, na kamwe sitalifikia hili somo.

Ee, mimi nina furaha mno kuwa Mkristo! Mimi-mimi-mimi-mimi nisingependa kubadilishana nafasi na mtu yeyote katika ulimwengu, siyo marais, wafalme. Kama wao wangelinipa mimi ulimwengu wote, waseme mimi ningeliishi miaka milioni; baada ya hapo nitakufa, baada ya miaka milioni. Lakini sasa, miaka milioni, mbona, haitakuwa chochote sasa, tunaendelea tu kuishi, hakuna kifo. Hivyo ni jambo kuu kuwa Mkristo!

20 Nilikuwa nikiongea juu ya Abrahamu! Hebu turejee nyuma. Sasa sisi ni Uzao wa Abrahamu kama tuko ndani ya Kristo. Na ndipo kama wewe ni Uzao wa Abrahamu, unayo imani ile ile Abrahamu aliyokuwa nayo, kwa sababu ilikuwa ni imani yake

tunayozungumza juu yake. Hasa katika kanisa sasa, ni Uzao wa kifalme wa Abrahamu. Kulikuweko na uzao aina mbili wa Abrahamu. Mmojawapo ulikuwa wa kimwili, Isaka; ule mwingine ulikuwa Kristo, ile ahadi. Hivyo kupitia Isaka, Israeli walibarikiwa; kupitia Kristo, yeye akafanyika baba wa mataifa. Unaona? Hivyo ule Uzao wa kifalme, huo ungelikuwa mkuu zaidi iliyoje kuliko uzao wa kimwili wa Abrahamu. Hivyo kama wewe uko ndani ya Kristo, wewe unao Uzao mkuu, mkuu zaidi ya aliokuwa Abrahamu, kwa sababu wewe unakuja kwa njia ya Uzao wa kifalme, Kristo. Kama ninyi mmekufa katika Kristo, basi ninyi ni watoto wa Abrahamu, na mnao Uzao wa Abrahamu na imani ya Abrahamu. Na imani ya Abrahamu ilikuwa katika Neno la Mungu pasipo kujali nini kilitukia. Yeye aliyaita hayo mambo yasiyokuwako kama kwamba yaliyokuwako, kwa sababu Mungu alisema hivyo. Ni ahadi iliyoje!

21 Sasa hebu turejee nyuma kiasi kidogo na tuwekee msingi mawazo yetu. Hebu turejee nyuma kwenye, kabla hatujafikia Yehova-yire, kwa Abrahamu. Hebu turudi nyuma, turudi nyuma kidogo katika Andiko. Hebu turejee nyuma kwenye sura ya 12. Tulisoma hapa katika sura ya 22. Hebu turejee nyuma kwenye sura ya 12, lile agano alilofanyiwa Abrahamu. Sasa, hilo agano, kulikwisha kuweko na matatu… maagano mawili.

Sasa, Mungu anakamilishwa katika tatu. Tunajua hizo tarakimu za Mungu. Ukamilifu, katika tatu; kuabudu, katika saba; na kumi na mbili; na arobaini, ni jaribu; hamsini, ni Yubile; na kadhalika, Mungu katika tarakimu Zake. Sasa, Mungu anakamilishwa katika tatu; kama Baba, Mwana, Roho Mtakatifu; kuhesabiwa haki, utakaso, ubatizo wa Roho Mtakatifu; na kadhalika.

22 Sasa, kulikwisha kuweko na maagano mawili. Mojawapo lilikuwa agano la Adamu. Mungu alifanya agano na mwanadamu, "Kama wewe utafanya, Mimi nitafanya." Na yeye akalivunja hilo. Ndipo Mungu akafanya agano na Nuhu; hilo lilikuwa agano la Nuhu, na hilo lilivunjwa.

Sasa Yeye anaweka agano la Abrahamu. Na agano la Abrahamu, kulingana na Mwanzo sura ya 12, hilo lilitolewa pasipo masharti. Kwa hiyo hilo ni la Milele, kwa sababu halina masharti. Siyo "Kama wewe utafanya, Mimi nitafanya." Yeye alisema, "Nimefanya! Mimi nimekwishakufanya hilo." Siyo "Mimi nitafaya hilo." "Nimekwishakufanya hilo!" Sasa hilo, ee, hilo, hilo linawekea imani msingi. Unaona, siyo…Mungu amedhamiria kumwokoa mwanadamu. Yeye alifanya agano, "Kama wewe utafanya, Mimi nitafanya," yeye alilivunja hilo. Lingine, "Ukifanya, Mimi nitafanya," yeye akalivunja hilo. Mwanadamu hawezi kushikilia agano lake, hivyo Mungu humwokoa mwanadamu kwa neema Yake, chini ya agano lisilo na masharti, agano lisilo na masharti. Loo, jamani! Halina mwisho kamwe, lilikuwa ndilo hilo lote; tatu, kamilifu. Nuhu, Abrahamu, na namaanisha…Adamu, Nuhu, na Abrahamu. Sasa, hiyo ndiyo sababu sisi ni watoto wa Abrahamu, hilo agano haliwezi kuwa na mwisho, kamwe halina mwisho, kwa sababu halina masharti. Hilo siyo…Hilo siyo kwa sababu wewe ulifanya kitu fulani; ni kwa sababu Mungu alifanya kitu fulani! Siyo kwa sababu wewe ulimchagua Mungu; Mungu alikuchagua wewe! Je, unaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina!"-Mh.]

23 Watu husema, "Ee, Ndugu Branham, nalimtafuta Mungu na kumtafuta Mungu!" Nawe hukumtafuta! Nachukia kukuambia wewe hilo, lakini hukumtafuta. Mungu alikutafuta wewe. Ilikuwa ni Mungu akikutafuta wewe.

Yesu alisema, "Ninyi hamkunichagua Mimi; Mimi niliwachagua ninyi. Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu, na wote Baba alionipa watakuja Kwangu." Sasa, ona, haikuwa hivyo. Hakuna mtu awezaye kujitukuza katika kitu chochote. Ni Mungu! Ee, ni zuri iliyoje kuona ile-ile neema halisi ya Mungu, jinsi hiyo ilivyo…

Na sasa watu wameuchukua Ujumbe wa neema na kufanya aibu kutokana na Huo! Kama kanisa langu la thamani na ninyi watu wa thamani wa Baptisti, mlipoichafua neema namna hiyo, kwa kweli mmeiingiza hiyo kwenye vurugu.

24 Mtu mmoja aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, "Ndugu Branham, sasa unajua wewe ulikuwa Mbaptisti mzuri."

Mimi nikasema, "Bado najisikia hivyo, lakini nimepanda juu zaidi kidogo."

Yeye akasema, "Vema, sasa tazama," kasema, "Abrahamu alimwamini Mungu, na

hilo lilihesabiwa kwake kuwa haki. Ni zaidi kiasi gani Abrahamu angeliweza kufanya isipokuwa kuamini?" Na yeye akasema, "Tunapomwamini Mungu, tunampokea Roho Mtakatifu!"

Nikasema, "Ni tofauti iliyoje na Mtakatifu Paulo? Mtakatifu Paulo alisema, katika Matendo 19, 'Je, mlimpokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?' Siyo, mlipoamini; 'tangu' mlipoamini!"

Yeye akasema, "Vema, Abrahamu alimwamini Mungu, ni hilo tu yeye angeweza kufanya."

Nikasema, "Kweli. Lakini ndipo Mungu akampa yeye mpango wa tohara, kama uthibitisho kwamba Yeye alikuwa amepokea imani yake.

25 Na kama Yeye kamwe hajakutahiri wewe bado kwa njia ya Roho Mtakatifu, Yeye hajapokea imani yako bado. Hilo ni sahihi. Hiyo ni tohara ya moyo na roho. Mungu hutoa Roho Mtakatifu kama uthibitisho kuwa Yeye amepokea imani yako. Sasa, kama ukiacha kuamini, na kuhangaika huku na huko; na kumwamini tu Mungu, Mungu atautahiri huo moyo. Na hilo hukatilia mbali kutokuamini kote, hutahiri ulimwengu na kutokuamini kote mbali na wewe; na ndipo unasimama, lile Neno pekee. Yesu alisema, "Kama mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu; basi ombeni lolote mtakalo nanyi mtapewa."

26 Hilo ndilo tatizo la kanisa leo. Liko chini ya msisimko, liko chini ya elimu, liko chini ya kanuni ya dini. Si ajabu, limesongwa mno! Hivyo tunahitaji tohara, ili kukatilia mbali hilo jambo lote. Turejee kwa Mungu na Neno Lake, na tuliamini hilo jinsi lilivyoandikwa, na tusibishane nalo. Tudumu tu na Hilo. Mungu aliweka ahadi, Mungu hutimiza ahadi Yake. Yeye hawezi kufanya chochote kingine bali kutimiza ahadi Yake, na abakie kuwa Mungu.

27 Sasa hili agano lisilo na masharti. Siyo "kama utafanya, Mimi nitafanya, bali Mimi nitafanya baadaye," au kitu fulani kama hicho; "Nimekwisha kukupa ile nchi, na Uzao wako baada yako!" Amina. Unaona, amekwishakulifanya hilo! Ni kazi iliyomalizika.

Wewe unasema, "Yeye alifanya hilo kwa Abrahamu." Ndiyo, siyo kwa Abrahamu pekee, bali kwa Uzao wake baada yake.

Na kama sisi ni Uzao wa Abrahamu, ni zao lililomalizika. "Hao ambao Yeye aliwajua tangu asili, Yeye aliwaita; hao ambao Yeye aliwaita, Yeye aliwahesabia haki; hao ambao Yeye aliwahesabia haki, Yeye amekwishakuwatukuza." Wewe unaogopa nini? Hilo ni sahihi. "Na mpingakristo, katika siku za mwisho," kulingana na Ufunuo, "aliwadanganya wote wakaao juu ya uso wa dunia, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwanakondoo" (tangu uamsho uliopita? Hapana) "kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu." Hiyo ni wakati jina lako lilipowekwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwanakondoo, wakati Mwanakondoo alipochinjwa. Mungu alinena Neno; Hilo lilikuwa katika mawazo Yake, katika wazo, Yeye alinena Neno na kila kitu kikatukia kwenye ule wakati tu. Huu ni Uzao wa Mungu tu ukidhihirika, ni hivyo tu, Maneno Yake yakija chini. Sasa, Nuru ya Mungu inapomulika kwenye huo, huo Uzao kwa haraka unaitambua Hiyo, kwa sababu Hiyo imezaliwa na Mungu. Ni Uzao wa Abrahamu, uliojulikana tangu asili na Mungu. Hiyo ndiyo sababu Nuru inamulika, ni ili kuudaka huo Uzao. Kama hiyo…

28 Tumekuwa na uamsho. Yoeli alisema. Tunahangaika mno juu ya mvua ya vuli, tulikuwa na harakati la kidini lililoitwa "mvua ya vuli," mvua ya vuli, mvua ya masika, mvua ya ndani, mvua ya nje. Nilikuwa nikisoma siku ile nyingine. Je, unajua mvua ya masika humaanisha nini katika neno la Kiebrania? Siwezi kulisema hilo sasa hivi; kamwe sikuliandika hilo, liliondoka akilini mwangu. Lakini mvua ya masika, mvua ya kwanza, humaanisha "mvua ya mafundisho." Mvua ya pili ni Roho anayekuja juu ya kile kilichofundishwa, na hutoa zao. Kwa nini tumekuwa na uamsho kama huu? Pentekoste, Baptisti, hiyo mito yote mingine imechipua machipukizi yake, kama Yesu alivyosema ingekuwa. Na tumetotoa nini? Wabaptisti walisema wao "wanao milioni zaidi katika mwaka 1944." Tazama Katoliki, jinsi wao walivyoongezeka. Yatazame madhehebu yote. Tazama Pentekoste. Tulifanya nini? Tulipanda mbegu za kidhehebu, tukavuna mavuno ya kidhehebu. Mbona, kanisa linapaswa kuwa na moto kwa ajili ya Mungu sasa hivi, kama kumekuweko na mbegu ya Neno iliyopandwa nyuma kule, na kutakuweko na ishara, maajabu, miujiza, na hilo kanisa lingekuwa pamoja, moyo mmoja, patano moja, na wakitembea kuelekea Sayuni, kwa ajili ya Unyakuo. Hilo ni sahihi. Tulifanya nini? Tulikuwa na hotuba za kiakili badala ya Neno. Tulikuwa na hoja dhidi ya Neno, na kila

kitu kingine.

29 Tunapaswa turudi nyuma kwenye Neno. Tunapaswa…Na tutafanya hilo! Mungu alisema, "Nitarejesha, asema Bwana, miaka yote ambayo tunutu na parare walikula." Hilo linakwenda kuchanua katika wakati wa jioni. Kutakuja mmoja mwenye Ujumbe, yeye atarejesha mioyo, au imani ya watoto irejee kwenye Imani ya akina baba. Yeye aliahidi hilo katika Malaki 4, kwamba Yeye angelifanya hilo, kuwarejesha hao tena.

Sasa, huyo siyo Eliya aliyetajwa katika Biblia; Yesu alisema katika Mathayo 11, "Kama mnaweza kulipoea hilo, Yohana pale alikuwa yule Eliya ambaye alikuwa aje," wa Malaki 3. "Tazama, namtuma mjumbe Wangu mbele za uso Wangu," Malaki 3, uone hilo.

30 Lakini kumbuka, Malaki 4, huo Ujumbe unakuja, "Siku ya Bwana ya kuogofya itakuja na itaiteketeza dunia yote, na wenye haki watatembea juu ya majivu ya waovu." Kamwe hilo halikutokea baada ya Yohana. Hapana, kama hilo lilikuwa hilo, basi Andiko limepoteza msimamo Wake, Hilo lilisema jambo fulani ambalo halikuwa hivyo. Tunayo miaka elfu mbili tangu wakati ule, ulimwengu haujateketezwa tangu wakati ule, hata kidogo. Wala wenye haki hawajatembea juu ya-ya majivu ya waovu. Lakini bado tunasubiri kuwa jambo fulani ambalo linakwenda kuhitaji Imani, na kurejesha imani ya watoto irejee kwenye Mti wa asili wa kipentekoste ule ambao tunutu aliula akaumaliza, madumadu. Dhehebu lao lote na kanuni ya imani ya dini iliula Huo na kuumaliza. Mungu alisema, "Nitarejesha hilo tena, katika siku za mwisho." Na Hilo litarejeshwa! Mungu atatuma Roho Mtakatifu kwa namna hiyo, juu ya Neno lililopandwa, ambaye atarejesha. Neno la Mungu ni Mbegu ambayo mpanzi alitoka kwenda kupanda.

31 Sasa, lile agano lilitolewa pasipo masharti! Sasa, Israeli, ile mbegu ya asili ilibadilisha hilo, na kulipoteza hilo katika Kutoka 19, wakati wao walipotengeneza kile kitu kibaya ili kuondoa neema, na kukubali sheria mahali pake. Ni kosa baya iliyoje ambalo Israeli walilifanya pale!

Tazama! Mungu, baada ya Yeye kufanya lile agano na Abrahamu, neema ilikuwa imekwisha kumleta nabii mkombozi kwa ajili yao kule chini katika Misri, ili kutekeleza neno la Abrahamu. Kumbuka Musa, chini ya kichaka, Mungu alisema, "Nimesikia kilio cha watu Wangu, na nakumbuka ahadi Yangu." Kabla hapajakuweko na sheria, neema ilitoa hilo. Neema ilikuwa imekwishatoa dhabihu kwa ajili ya hatia yao, mwanakondoo. Neema imetoa agano, tohara, ilikwishatolewa, kabla ya hilo lote. Neema ilikuwa imetoa Nguzo ya Moto ili kuwaongoza wao, kumfuata nabii, usalama kwamba nabii alikuwa amewaambia ile Kweli, ilikuwa ni Neno ambalo yeye alikuwa analizungumzia. Wao walijua kuwa Mungu aliahidi hilo, na hapa kulikuweko na Nguzo ya Moto ikithibitisha hilo. Ni usalama mara mbili ulioje! Amina. Neema imefanya hilo!

Lakini wao walihitaji kitu fulani kwa ajili yao wenyewe ambacho waliweza kufanya, wawe na kanuni zao wenyewe za imani za dini na madhehebu, chochote kile, wafanye Mafarisayo, Masadukayo, na kitu fulani walichoweza kufanya wenyewe.

Mwanadamu siku zote anajaribu kujiokoa mwenyewe. Huwezi kufanya hilo! Mungu amekwishakufanya hilo. Inakupasa tu kulipokea hilo na kuliamini hilo.

32 Nguzo ya Moto ili kuwaongoza wao na kuwaelekeza wao, kuwaongoza wao katika Njia. Nguvu ambayo, neema ilikuwa imewapa Nguvu ili kumwangamiza adui yao na kuwafanya wao wawe huru. Ile Nguvu walikwishapewa tayari. Wao walivuka Bahari ya Sham. Wao walikuwa wamekwishampiga Farao. Wao walifanya haya mambo yote kwa neema. Na ndipo wao wakabadilisha na neema kwa sheria, lakini hilo halihusiani chochote na Uzao wa kifalme wa Abrahamu.

Ule Uzao wa kifalme umejaribu kufanya kitu kile kile, umerejea nyuma chini ya aina fulani ya kanuni ya imani ya dini badala ya kuchukua neema na Neno, na kuliamini Hilo. Wao walirudi nyuma. Lakini utakuja Uzao wa kifalme; tutafikia hilo baada ya kitambo kidogo, tuendelee mbele kidogo.

33 Hebu turejee nyuma sasa kwenye Mwanzo 12. Mungu alimwita Abrahamu kwa njia ya neema. Siyo kwa sababu yeye alikuwa mtu tofauti; yeye alikuwa Abrahamu tu, mtu wa kawaida tu. Siyo kwa sababu yeye alikuwa kuhani au mtu mashuhuri; yeye alikuwa mkulima tu. Yeye alikuja chini kutokea mji wa Mnara wa Babeli, pamoja na baba yake, na walikuwa wamekwenda Ukaldayo, Uri ya Ukaldayo. Na, kule, alikuwa mkulima, labda alilima wakati wa mchana na kukuza chakula chake. Yeye alikuwa amemuoa binamu yake, Sara. Nao hawakuwa na watoto, na Abrahamu alikuwa na umri wa miaka sabini na

tano Mungu alipomwita yeye, na Sara alikuwa na umri wa miaka sitini na tano.

Na Mungu alimwambia Abrahamu wakati Yeye alipomwita, Yeye alisema, "Nakwenda kukufanya wewe baba wa mataifa," na kwenda kumpa yeye mtoto kwa njia ya Sara. Sasa, Abrahamu alikuwa ni mgumba. Na Sara alikuwa, vema, miaka sitini na tano, Sara alikuwa amekwishakupita kwa miaka kumi au kumi na tano umri wa kuweza kuzaa. Abrahamu alikuwa ameishi na Sara tangu akiwa na kama umri wa wa miaka kumi na sita au kumi na saba, binamu yake. Na, wao, yeye alikuwa amekuwa mume kwake miaka yote hii hadi yeye alipokuwa na umri wa miaka sabini na tano, na Sara alikuwa na umri wa miaka sitini na tano, na ndipo Mungu akaja chini na kusema, "Ninakwenda kukupa wewe mtoto, kwa njia ya Sara." Na yeye hakuyumba kwenye hiyo ahadi ya Mungu, bali aliiamini hiyo!

34 Ungeweza kuwazia mwanamume mzee, mwenye umri wa miaka sabini na tano, na mwanamke, miaka sitini na tano, wakienda chini, wakitetemeka, chini kwenda kwa daktari, na kusema, "Daktari, nataka wewe uandae hospitali sasa. Sisi tunaweza kukuita usiku wowote, kwa sababu, unajua, tunakwenda kuwa na mtoto."?

Daktari angelisema, "Naam, ndiyo, bwana, ninyi ni…Lo, lo, lo!" Mara tu walipokuwa wakipiga simu, waseme, "Ni bora tumfuatilie, huyu ana tatizo fulani."

Na kila mtu anayemchukulia Mungu alivyo kwenye ahadi Yake anachukuliwa, na ulimwengu kuwa, "mwendawazimu." Paulo alisema, "Katika njia inayoitwa 'uzushi," hiyo ndiyo njia ninayomwabudu Mungu wa baba zetu." Uzushi wa kidini ni "wendawazimu," tunajua. Ni upuuzi kwa akili za kimwili. Imani ni wendawazimu kwa kila mtu isipokuwa Mungu na yule mwenye hiyo imani. Hilo ni sahihi

35 Lakini Mungu alimwahidi Abrahamu, na Abrahamu aliamini hilo. Kamwe yeye hakusema, "Mungu, hilo litakuwaje?" Yeye alisema, "Sawa, Mungu, mimi naamini hilo." Na naweza kumwona yeye akienda nyumbani, akisema, "Sara, hebu twende chini na tuwe na yadi kadhaa za nepi, na tuwe na pini kadha, na tuwe na viatu fulani. Tunakwenda kuwa na mtoto." Loo, jamani!

Kwanza siku thelathini zilipita, au siku ishirini na nane. "Unajisikiaje, mpenzi?"

"Hakuna tofauti."

"Mungu abarikiwe, tunakwenda kuna naye, kwa vyovyote!"

"Wewe unajuaje?"

"Mungu alisema hivyo!"

Baadhi yetu tunaweza kuombewa usiku mmoja, na kuketi katika mkutano ambapo Roho Mtakatifu anashuka; na asubuhi inayofuata, kama hatuko wenye afya, vema, wenye nguvu, "Mimi-mimi bado ni mgonjwa, tumboni mwangu kidogo. Siwezi kusogeza mikono yangu tena." Uzao wa Abrahamu, haukutikisika kwenye ile ahadi ya Mungu kwa kule kutokuamini?

36 Kitu fulani kinakuja kanisani, yule Mwovu anaweza kuingia miongoni mwa kundi la watu wazuri na kuingia pale na kwenda kulipiga hilo kusanyiko huku na huko, kitu cha kwanza unajua, baadhi wanasema, "Loo, nakwenda kuachana na hiki Kitu cha kale, hapakuweko na lolote kwenye Hicho hata hivyo." Uzao wa Abrahamu? Jamani, jamani! Ufa wa kwanza yule Mwovu anaoweza kukuonyesha, wewe unaachana na Hilo. Hilo linaonyesha wewe hukuliamini Hilo hapo kwanza.

Yesu alisema, "Ule Ufalme unafanana na mtu aliyechukua wavu, na kwenda baharini na kuutupa baharini. Yeye alipoingia ndani, alikuwa na kila kitu." Hilo ni sahihi.

Hilo ndilo-hilo ndilo uamsho hudaka. Nini kilichoko ndani ya wavu? Una vyura, buibui, kasa, samaki mtambaaji, nyoka, na samaki. Si muda mrefu sana hadi yule kasa anaposema, "Vema, hapa siyo mahali pangu," anakwenda moja kwa moja katika tope. Yule buibui wa kale wa majini alitazama huku na huko, na kusema, "Loo! Siwezi kuwa na mchezo wa karata hapa." Hivyo yeye anakwenda chini katika tope tena, kama nguruwe kwenye matope yake na mbwa kwenye matapiko yake. Hilo ni sahihi. Na ndipo Uzao wa Abrahamu? Loo, jamani! Aibu kama hii!

Uzao wa Abrahamu unaliamini Neno la Mungu!

37 Unaketi nyuma pale na kusema, "Naam, Mungu abarikiwe, mimi ni Mpentekoste!" Na mtu fulani anahubiri jambo fulani juu ya Neno, likiwa limeandikwa pale pale.

"Haleluya, mimi siamini Hilo. Hapana, bwana." Uzao wa Abrahamu? Loo!

Sasa, kama hilo ni upuuzi, bila shaka, wewe huamini hilo. Lakini kama Hilo ni Neno, Hilo ni ile Kweli! Hilo ni sahihi. Uzao wa Abrahamu hushikilia kwenye hilo Neno na si kitu kingine.

38 Mwezi mwingine umepita. "Sara, mpenzi, unajisikiaje sasa? Unajua, siku nyingine ishirini na nane zimepita, unajisikiaje?"

"Hakuna tofauti, mpenzi."

"Utukufu kwa Mungu! Huo ni mwujiza wa miezi miwili mkuu zaidi kuliko ulivyokuwa kama lilitukia mwezi uliopita."

Mwaka ukapita. "Je, niondoe hizi buti ndogo?"

"Hapana, bwana, ziweke pale. Tunakwenda kupata mtoto!"

"Unajuaje unakwenda kumpata?"

"Mungu alisema hivyo! Hilo limekwisha."

Baada ya miaka ishirini na tano kupita. "Unajisikiaje, Sara?"

"Hakuna tofauti."

"Utukufu kwa Mungu! Ni miaka ishirini na tano zaidi ya mwujiza sasa!" Yeye hakuyumba kwenye ahadi ya Mungu kwa kutokuamini bali alikuwa imara, akishikilia Neno la Mungu; na kuita hayo mambo yasiyokuwapo kuwa bayana, kama vile yalikuweko. Kwa nini? Mungu alisema hivyo! Loo, jamani!

39 Uzao wa Abrahamu leo, mbona, ule tunaoita Uzao wa Abrahamu, ni dhaifu kuliko mchuzi uliotengenezwa kutokana na kivuli cha kuku aliyedhoofika kwa njaa. Ndiyo, bwana.

Mungu anataka Wakristo walio imara wanaolichukua Neno la Mungu, waishi au wafe. Ni kitu kile kile. Amina. "Mungu alisema hivyo!" Huo ni Uzao wa Abrahamu, uliozaliwa kwa Roho na Neno la Mungu. Hilo ndilo linalosimama.

"Mbingu na nchi zitapita, lakini Neno Langu halitapita kamwe." Hilo ndilo jambo lenyewe. Kile Mungu alichoahidi, Mungu anaweza kufanya. Mungu hashindwi. Yeye hawezi kushindwa. Kuna kitu kimoja pekee ambacho Mungu hawezi kufanya, na hicho ni kushindwa. Yeye hawezi kushindwa, hicho ndicho kitu pekee Yeye hawezi kufanya. Lakini Yeye hawezi kushindwa. Mungu alipoahidi hilo, hiyo ni ile Kweli, Hilo linabaki pale daima. Hilo linakuwa limekwisha daima. Mungu anaponena Neno, hilo tayari limekamilika daima.

40 Huu ulimwengu uliumbwa kwa njia ya Neno tu la Mungu. Yeye alisema tu, "Na kuweko," na kukaweko. Amina. Hiyo hiyo taka ulioketi juu yake jioni hii, hiyo hiyo mbao uliyokalia jioni hii, si chochote bali lile Neno la Mungu lililodhihirishwa. Haleluya!

Najisikia wa kidini ninapowazia juu ya Abrahamu, nikijua kuwa tunaweza kuwa Uzao wake, ule Uzao wa Abrahamu pamoja na hizi ahadi zote. Siyo tu kuifanya hiyo kuwa hakika, Mungu aliinua mkono Wake juu, akaapa kwa Yeye Mwenyewe, kuwa angelifanya hiyo. Kiapo ni, siku zote, agano linathibitishwa na kiapo, na Mungu aliapa kwa Nafsi Yake Mwenyewe kwa sababu hakuna wa juu zaidi wa kuapa kwa yeye. Yeye aliapa kwa Nafsi Yake Mwenyewe, kuwa angelifanya hilo.

Sasa kile ulimwengu, jinsi, nini-tatizo letu ni nini? Ahadi kama hiyo! Imani iliyojengwa kwenye kitu fulani kama hicho, imani iliyojengwa! Neno lililoahidi haya mambo katika siku za mwisho, na hapa tunayaona yakitukia moja kwa moja mbele zetu, na bado tunajitweza. Uzao wa Abrahamu? Loo, jamani! Nataka ninyi mshikilie kwenye hilo, "Uzao wa Abrahamu."

41 Mwanzo 12, kile Mungu alichohitaji kwa Abrahamu kilikuwa utenganisho kamili.

Sasa, leo, wao wanataka wachanganyaji. "Ee, tunapomchagua mchungaji, inampasa yeye awe na nywele zilizosokotwa, na awe ametoka moja kwa moja Hollywood, unajua, na aweze kusema, "ah-mina" kwa uzuri zaidi, na anayevaa nguo zilizo bora zaidi ya zote, na anayeendesha Cadillac lililo kuu, na-na kadhalika namna hiyo, na yeye awe mchanganyaji mzuri. Yeye hufanya hili. Na awe anakunywa pombe mara chache pamoja nasi, ili awe mtu mwenye kuweza kuchanganyika na watu wengine. Yeye ahudhurie kwenye karamu ya kadi ya akina bibiye wazee, na wao

hushona na kufuma, na kufuma na kushona, na kuzungumza juu Binti Fulani na Fulani, na kadhalika, unajua, na yote namna hiyo. Na inapasa wao wawe namna ile ya wachanganyaji."

42 Mungu alisema, "Nitengee Paulo na Barnaba!" Amina. Utenganisho! "Tokeni miongoni mwao na msishiriki vitu vyao vilivyo vichafu!" Mungu anataka utenganisho, kuangamiza dhambi kabisa. Jitenge!Hilo ndilo tatizo leo, sababu hatuwezi kuwa Uzao wa Abrahamu, hatuwezi kujitenga wenyewe na amri za sharti za kanisa na kanuni za imani za dini, na kadhalika, unaoitwa Ukristo, kwa Neno lililo hai. Jitenge mwenyewe na kutokuamini kwako, na uamini Neno la Mungu. Mungu atalifanya Hilo lidhihirike kwako. Sawa.

Mwanzo 12, Mungu alisema, "Jitenge mwenyewe na jamaa yako na kila kitu kilichokuzunguka." Ee, jamani, hatuwezi kujitenga wenyewe na kucheza karata! Loo!

43 Niliingia kwenye mgahawa leo, wakati ndugu alipoingia ndani pale. Nikamtazama tineja fulani mwenye utovu wa adamu akiingia pale. Na mke wangu na mimi tulikuwa tunakula, na nikawaza, "Mungu atukuzwe! Hebu tuharakishe, mpenzi, kabla mtu fulani hajaingia ndani." Na tineja fulani akaingia pale, akinywa kwa sauti pale. Ningeliogopa kukutana na yule mvulana katika giza. Na yeye aliweka mtambo wa sindano ndani pale, au rekodi, na kuanza kucheza kile kitu cha kale cha muziki wa jazi wa kale, na-na akiwa amesimama pale, akienda namna hii, unajua, akijipiga mwenyewe namna ile. Nikasema, "Kwa ajili ya wema, rehema…"

Meda alisema, "Usi-usiende pale kulipa ile ankara. Subiri papa hapa, hebu mimi niende pamoja nawe." Yeye aliogopa.

44 Mtu yeyote katika hilo, vitu kama hivi tulivyo navyo leo, taifa la Kikristo, ee, ni kitu cha jisi gani! Utenganisho! Asilimia tisini ya hao huimba katika kwaya, akina Elvis Presley, na Pat Boone, na wote hao, na Peabody Ernie, lolote wamwitalo yeye chini pale. Mbona, ni baya zaidi kuliko Yuda Iskariote! Yuda Iskariote aliuza, na kupata vipande thelathini vya fedha; Elvis alimpiga, yeye analo kundi la magari ya Cadillac na umaarufu mwingi. Na kwa sababu hawa watoto wadogo wanaona yote yanayoendelea, husema, "Yeye ni wa kidini mno." Huyo ni yule Mwovu! Kabisa! Mungu havumilii kitu kama hicho. Huyo ni kipofu. Mko hapa katika siku za mwisho.

Rejeeni kwenye Neno, "Jitengeni wenyewe na mambo maovu, na msiguse vitu vyao. Mimi nitawapokea ninyi."

45 Ile Injili, tunahitaji kuishika Hiyo kwa mikono mitupu! Siyo tukiwa tumevaa glovu fulani za kidini, tukimpigapiga mtu fulani mgongoni kwa kumpongeza, hilo linakuwa na kiota kilichojaa mayai yaliyooza tena, kumfanya mtu fulani kiongozi katika wilaya, au mwangalizi wa eneo, askofu, au kitu fulani kingine. Yeye ana ninii… Unawezaje kuwa na imani wakati unaheshimiwa, mnaheshimiana ninyi kwa ninyi? Tunamtazama Mungu, na Yeye pekee! Heshima huja kutokea kwa Mungu. Yeye Ndiye Aliye. Tunamheshimu Yeye kwa kushikilia Neno Lake kama tochi, na tukitembea kama mwanamume au mwanamke mbele za Mungu.

[Sehemu tupu katika kanda-Mh.] Walivuka pale mtoni na kwenda katika ile nchi, Mungu alisema, "Abrahamu, nitakupa hiyo yote sasa, lakini hujanitii Mimi kikamilifu."

46 Na jambo la kwanza unajua, kukaja ugomvi mdogo juu wachungaji wa mifugo, na miongoni mwa watunzaji mifugo wao, katika Mwanzo 13 (kulitukia nini?), wachungaji wa mifugo wa Lutu na wachungaji wa mifugo wa wa-wa Abrahamu. Mtazame Abrahamu, tendo la kindugu, yeye alisema, "Kusiwe na mabishano kati yetu. Sisi ni ndugu." Lutu aliwakilisha kanisa vuguvugu. Na yeye alisema, "Tazama nje, chukua uchaguzi. Chochote utakacho, endelea na ukichukue. Ukienda mashariki, mimi nitakwenda magharibi, na kadhalika. Au, ukienda magharibi, mimi nitakwenda mashariki. Ukienda kaskazini, nitakwenda kusini, na kadhalika. Uchukue uamuzi wako." Na Lutu alikwishakuwa chini katika Misri na alikuwa na jicho la umaarufu kidogo, alikuwa na fedha kidogo mfukoni mwake…

47 Hapo ndipo kanisa lilipokosea. Nasema hili kwa unyenyekevu, ndugu. Kanisa la Kipentekoste lingekuwa bora zaidi likiwa na kinubi, nje kule kwenye kona, pamoja na wanaume na wanawake wa mtindo wa kale, pamoja na ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuliko ambavyo wangekuwa katika hizi sehemu kuu na kubwa za kuhifadhia mabaki ya vitu vitakatifu na nyumba za kuhifadhia maiti wanakoishi leo chini ya huu upuuzi na vitu

kama hivyo. Hilo ni sahihi. Wao wanataka kutenda kama hao wengine. Hapo ndipo tulikofikisha hilo. Kwa nini hamkubakia jinsi mlivyokuwa, jinsi Mungu alivyowaanzisha? Kitu kile kile mlichogombania, na mligeuka nyuma na kufanya kitu kile kile.

Hivyo ndivyo Lutu alivyofanya, alikwenda chini katika Misri na, kitu cha kwanza unajua, yeye aliweka macho yake juu ya Misri. Na ndipo akatazama kule na kuiona Sodoma, anasa, akalichukulia hilo kirahisi. Na yeye alikwenda kuelekea mashariki-kuelekea…Kumbuka, alikwenda mashariki badala ya kwenda magharibi pamoja na Abrahamu. Yeye alikwenda mashariki kwa sababu hiyo ilikuwa njia ya anasa. Yeye alikwenda kuelekea mashariki.

48 Hivyo ndivyo kanisa limefanya leo, unaona, wao walirejea nyuma. Kama nilivyosema jioni iliyopita, jua huchomoza katika Mashariki na linakwenda Magharibi. Na Mwana wa Mungu alitembelea Mashariki kwanza, na amekwenda kuelekea magharibi. Wao walitembea, kupitia miaka miaka elfu mbili. "Lakini kutakuweko Nuru katika wakati wa jioni," huyu nabii alisema. Badala ya kumfuata Mwana alikoelekea, wao walirudi pale Mwana alikokuwa. Leo inatokea unasema jambo fulani juu ya uponyaji wa Kiungu, juu ya unabii, juu ya karama tisa za kiroho, au kitu fulani; "Hebu turudi nyuma na tuone kile Moody alichosema, kile Sankey alichosema, kile Knox alichosema, kile Calvin alichosema." Wao waliishi katika siku wakati Mwana alikuwa anang'aa kule; sisi tunakwenda kuelekea kwenye ukamilifu!

49 Mwanasayansi wa Kifaransa alisema, takriban miaka mia tatu iliyopita, alithibitisha hilo kwa kuviringisha mpira kuzunguka tufe, yeye akasema,"Kama mtu yeyote angewahi kwenda kwa mwendo kasi wa maili thelathini kwa saa, nguvu ya uvutano ingewachukua wao waondoke duniani." Alithibitisha hilo kisayansi. Unafikiri sayansi itawahi kunukuu hilo? Hapana, bwana! Wao wanao hao wanaokwenda kama maili elfu mbili kwa saa, wakijaribu kuwafanya hao waende mbali zaidi. Wao hawatazami nyuma kwenye hilo.

Lakini wahudumu, "Sisi tutatazama nyuma na tuone kile Moody alichosema, kile Sankey alichosema." Hapo ndipo Mwana alikokuwa. Hapa ndipo Hilo liliko leo! Hilo liko kwenye Pwani ya Magharibi, katika wakati wa jioni, haleluya, likitoa Nuru za jioni! Siyo kurejea nyuma kwa kuhesabiwa haki kwa Luther au utakaso wa Wesley; bali tuko kwenye siku ya mwisho, amina, wakati Nuru za jioni zinang'aa, wakati tuko kwenye wakati wa mwisho. Mfuate Mwana.

Lakini Lutu alirejea nyuma, kwa sababu ilikuwa rahisi, anasa. Mtazame Bibi Lutu alipofika nyuma kule. Mbona, ni lazima yeye alifanyika kuwa malkia wa zile jamii za jiji. Lutu alifanyika kuwa meya. Ee, ndugu, walililiunda hilo, mbona, namaanisha kusema!

Hivyo ndivyo watu wamemchukulia Bibi Lutu leo. Tazama jinsi ambavyo watu wetu wanavyotenda leo. Tazama watu wetu katika makanisa, litazame tu hilo. Watazame wanawake wetu, watazame wao leo.

50 Mimi-mimi nilikuwa katika Hollywood ile wakati ule…au katika Los Angeles, hivi karibuni, nilikuwa nikimsubiri Ndugu Arganbright ili aje. Na pale alisimama msichana, akaja juu pale. Nilitazama, na nikayumba. Nikamtazama. Nikawaza, "Mimi ni mmishenari. Nimeona tauni, nimeona ukoma, lakini kamwe sijawahi kuona kitu chochote kama kile." Alikuwa na mojawapo ya huku kukata nywele mtindo wa kukata nywele utosini kama ukoka, hizi, mnajua,, mnajua, kile mnachoita, ilionekana kama kukata nywele utosini kama ukoka, mnajua, yule-yule Bibiye wa Kwanza, naam, kama Yezebeli, namna hiyo. Na yeye alikuwa amejipaka rangi ya samawi na kijani; na huenda alikuwa awe mwanamke mwenye sura nzuri; lakini hivyo vitu vyote juu yake, yeye alionekana kama Hotentoti wa Kiafrika. Nilifika pale, nilikuwa ninakwenda kumwombea huyo mwanamke. Nikawaza, "Bibiye, kama hutajali, mimi huombea wagonjwa. Kamwe sikuwahi kuona kitu chochote kama kile. Niambie hicho ni kitu gani." Na ndipo mwanamke mwingine akazungumza naye, na yeye alikuwa vivyo hivyo. Loo, jamani!

Ee, unasema, "Huyo alikuwa Mpresibiteri." Mpentekoste! Hakika.

51 Na Biblia ilisema, "Ni kitu cha aibu kwa mwanamke kukata nywele zake." Yeye anafanya hilo, anatia aibu kichwa chake. Yeye anatia aibu malaika, malaika wa Nuru. Malaika wa Makanisa Saba, yule anayeleta Nuru atadumu na Neno. Kutia aibu! Yeye anapaswa kuwa na nywele kichwani mwake. Jamani, kitu kama hiki! Na ilikuwa hapo zamani ni makosa kwa wao kufanya hilo. Katika-katika Pentekoste ya kwanza, ilikuwa ni makosa. Kulitukia nini? Mlitembea vizuri, kulitukia nini?

Na baadhi ya wanawake wetu wa Kipentekoste huvaa magauni yanayoonekana kama mavazi yaliyoshikana na ngozi, nje hapa mahali fulani wakijaribu…Hilo ni sahihi! Mimi sisemi hilo kwa ajili ya mzaha. Hapa siyo mahali kwa ajili ya kufanya mzaha. Hii ni mimbara.

Mwanamke fulani aliniambia jioni moja. Niliwaambia jinsi wao walivyokuwa wamevaa. Nikasema, yeye akasema, "Mimi sivai kaptula, Mimimimi-mimi huvaa suruali."

Nikasema, "Hilo ni baya zaidi ya yote. Mungu alisema, 'Mwanamke atakayevaa vazi limpasalo mwanamume, ni chukizo mbele za Mungu.'" Sawa!

Na hebu nikuambie jambo fulani, bibiye, wewe, mwanamke kijana, unayejivalisha mwenyewe nje huko, unakwenda kujibu penye siku ya hukumu kwa kufanya uzinzi.

Unasema, "Mimi ni msafi tu kama yungiyungi."

52 Naam, lakini Yesu alisema, "Yeyote amtazamaye mwanamke ili kumtamani, amekwishakuzini naye tayari moyoni mwake." Unaweza ukawa hujafanya hilo tendo. "Yeyote aliye na hasira na ndugu yake pasipo sababu, amekwishakuua tayari." Unaona, kitu pekee unachopaswa kufanya. Na kama huyo mwenye dhambi anakutazama jinsi ulivyovaa, akiwa amevutiwa kupindukia na jinsi ulivyo, kutazama nyuma, na kusukumiza nje, na kusukumiza ndani, na kuvaa aina hizo za nguo, ndipo unakwenda matembezini. Sasa sikiliza, hiyo siyo mizaha! Hii ni Injili! Na wewe unafanya namna ile, na mwenye dhambi fulani anakutazama na kukutamani. Penye siku ya hukumu, yeye atakapojibu kwa ajili ya uzinzi, ni nani aliyesababisha hilo? Wewe ulisababisha. Wewe utajibu kwa ajili ya hilo kwa sababu ulijiweka mwenyewe namna hiyo.

53 Mbona, unasema, "Wao-wao hawatengenezi aina nyingine za nguo." Wao wanatengeneza mitambo ya kushona, na bado wanauza bidhaa. Huo siyo udhuru hata kidogo! Ni kwa sababu mmeondoka na kwenda mbali na Neno! Hilo siyo haliwafurahishi. Hilo ni gumu.

Mhubiri fulani mashuhuri alikuja siku ile nyingine, na kuweka mikono yake juu yangu, akasema, "Ninakwenda kuweka mikono yangu juu yako na kuutoa uovu nje."

Nikasema, "Nini?"

"Unapozungumza juu ya wanawake namna hiyo." Kasema, "Watu wanakuchukulia wewe kama nabii."

Na kasema, mimi nikasema, "Mimi siyo nabii."

Yeye akasema, "Wao wanakuchukulia wewe hivyo, Ndugu Branham." Na akasema, "Wewe unapaswa uwe unafundisha hao watu, hao wanawake, jinsi ya kupata baraka kuu za kiroho. Na uendelee kuwaambia juu ya wao kukata nywele zao na vitu kama hivyo. Wao hawatasikiliza hilo."

Nilisema, "Mimi najua hilo."

Kasema, "Kwa nini huwafundishi wao mambo makuu zaidi?"

Nikasema, "Nawezaje kuhubiri, kuwafundisha wao aljebra wakati hata hawajui kusoma, lau hata uadilifu wa kawaida?"

54 Na wewe mwanamume utakayemruhusu mwanamke wako atende namna hiyo, nina heshima yako ya wewe kuwa mwanamume Mkristo, Uzao wa Abrahamu. Amina! Ni bora niliache hilo, nitawafanya ninyi nyote msimame na kwenda nyumbani. Vema. Mojawapo ya siku hizi unakwenda kushindwa kupata kitu fulani kule Juu.

Unasema, "Hilo halileti tofauti yoyote." Hilo lilileta kwa Paulo. Hilo lilileta kwa Mungu, katika Bustani ya Edeni. Biblia ilisema kuwa mwanamke anapaswa kuwa na nywele ndefu! Na bila hizo, wewe upo wapi? Vema, unasema, "Hilo halifanyi tofauti yoyote." Biblia ilisema hilo linafanya! Usimruhusu yule Mwovu ahojiane nawe, na kukuambia wewe, "Hilo ni la kisasa, ni sawa." Hilo siyo sawa! Unasema, "Mimi sikujua hilo hapo kabla." Unajua hilo sasa. Unaona? Chunguza hilo na uone kama ni sahihi. Nitaliacha hilo, unaona. Sawa.

55 Mwanzo 13, kisasa, loo; rejea nyuma pale Mwana alikokuwa, siyo pale Mwana aliko; pale Mwana alikokuwa, hata hivyo.Nawazia, jinsi ambavyo mke wa Lutu, alivyoingia katika jamii.

Hivyo ndivyo kwamba tunaingia katika jamii. Hivyo ndivyo sisi Wapentekoste tulivyoingia katika hilo. Tunafanyika, tukaunda shirika dogo la dini hapa, na moja dogo lililo kinyume, moja dhidi ya lingine, na dhidi ya hili, na wao wanaunda…Mnapokea kitu chochote. Hilo ni sahihi kabisa.

56 Samweli alisema nini wakati Israeli walipotaka ku-walipotaka kuwa na mfalme, walimtaka Sauli awe mfalme? Samweli alikuja kwao, na kusema, "Je, niliwahi kuchukua fedha yenu kwa ajili ya kuishi? Je, niliwahi kuwaambia ninyi lolote katika Jina la Bwana isipokuwa lilile lililotukia?"

Ee, wao walisema, "Hakika, wewe ni nabii wa Mungu. Wewe ulituambia ile Kweli, na kile ulichosema kilitukia, lakini sisi tunamtaka mfalme, kwa vyovyote."

Na wakati mlipoanza kuyaachia mambo , na kuruhusu hili na lile, na kila kitu kingine kiingie ndani namna hiyo, mlifanyika wa kisasa. Na kanisa ni kama tu hizo jumuia nyingine leo. Kile tunachohitaji ni kufanya usafi wa nyumba wa Kipentekoste! Hilo ni sahihi kabisa. Amina. Ni aibu Mbaptisti kuweza kukuambia wewe hilo, sivyo? Lakini hiyo ni ile Kweli. Sawa! Mimi naamini Biblia, naamini Neno la Mungu ni sahihi. Vema.

57 Abrahamu, ndipo Abrahamu akachukua ninii…katika aya ya 14 ya sura ya 13, baada ya Lutu kujitenga mwenyewe, na Abrahamu kumtii Mungu kikamilifu, ndipo Mungu akaja kwake. Sasa Yeye yuko tayari kumbariki Abrahamu.

Na hadi kanisa la Pentekoste liondokane na kanuni zake zote za imani za dini na amri za sharti za kanisa, na kule kutenda kama ulimwengu na kuonekana kama ulimwengu, na kuzungumza kama ulimwengu, na kukaa nyumbani Jumatano usiku ili kutazama kile kipindi cha televisheni cha Tunampenda Susie badala ya kuja kwenye mkutano wa maombi, na vitu kama hivyo, mkilipa mafungu yenu ya kumi kwa mhubiri fulani nje hapa juu ya aina fulani ya kipindi cha redio ili kukifanyia mzaha kitu kile kile mnachokisimamia, hilo ni sahihi, na aina hizi zote za mambo yanayofanywa katika jina la pentekoste, ni aibu!

58 Huwa ninawahubiria Wanaume Wafanyabiashara wa Kikristo, kimataifa. Kuna wengi wao walioketi hapa sasa. Hapa usiku ule mwingine, hilo limekuwa, hapa takriban mwaka mmoja uliopita, mimi nilikuwa Jamaica. Nao walikuwa na watu wote mashuhuri wa vile visiwa ndani mle usiku mmoja, na hawa watu wakisimama, wakishuhudia, "Utukufu kwa Mungu! Mimi nilikuwa mwanamume mfanyabiashara mdogo chini kwenye kona. Haleluya, ninayo magari ya Cadillac manne sasa. Utukufu kwa Mungu!"

Na nilirudi juu kule hadi Flamingo Hoteli ya wasafiri jioni ile, nikasimama pale, nikasema, "Nawaonea aibu!" Nikasema, "Ninyi watu hapa kumwakilisha Kristo, ukijaribu kumwambia mwanamume mfanyabiashara ni kiasi gani ulicho nacho, yeye anacho zaidi ya ulicho nacho au utakachowahi kuwa nacho." Hilo ni tofauti kwa kiasi kikubwa na jinsi wapentekoste wa kwanza walivyokuwa. Upentekoste wa kwanza uliuza ulichokuwa nacho, na kugawa miongoni mwa masikini, na kwenda na kuhubiri Injili. Sawa!

59 Mswidish fulani mdogo mwimbaji kutokea Chicago, sitataja jina lake. Yeye ni ndugu yangu wa thamani. Yeye alisimama wima, akasema, 'Ndugu Branham, ingawa wewe…Sisi tunaamini wewe kuwa ni nabii, lakini nitakuambia sasa hivi, 'Unakosea.'"

Nikasema, "Niambie mahali gani, ndugu."

Yeye akasema, "Vema, hao watu waliuza vile walivyokuwa navyo, na kuweka penye miguu ya mitume, na kukigawa hicho." Yeye akasema, "Hilo lilikuwa tendo baya zaidi walilowahi kufanya."

Nikasema, "Je, wewe unamaanisha kuniambia Roho Mtakatifu hufanya tendo la makosa?"

Na yeye akasema, "Hilo lilikuwa kosa. Nitakuthibitishia hilo."

Nikasema, "Kwa nini?"

Kasema, "Basi wakati dhiki ilipokuja, wao hawakuwa na mahali pa kwenda. Wao walitangatanga, kila mahali."

"Kabisa katika mapenzi ya Mungu, wakihubiri Injili kokote walikokwenda. Wao hawakuwa na mahali pa kurejea." Mungu hafanyi makosa. Sawa! Ee, hilo ni tofauti iliyoje; hiyo pentekoste iliyokuweko, na Pentekoste iliyoko. Naam, hilo ndilo jambo

lenyewe.

60 Baada ya Abrahamu kujitenga mwenyewe na Lutu, kile tu hasa Mungu alichomwambia afanye. "Tenga kila dhambi inayotulemea sisi, toa nje kila kitu!" Pale, ndipo Mungu aliposema, "Abrahamu, sasa wewe ni mrithi wa vitu vyote. Tazama mashariki, tazama magharibi, tazama kaskazini, tazama kusini, tembea kote kwenye nchi, yote ni ya kwako!" Amina.

Unatenga jambo lako, mwenyewe mbali na dhambi, kutokuamini. Kuna dhambi moja pekee, na hiyo ni kutokuamini. Kufanya uzinzi siyo dhambi, kunywa pombe siyo dhambi, kusema uongo siyo dhambi; hizo ni ishara zinazoashiria kutokuamini. Kama wewe uliamini, usingelifanya hayo mambo.Hakika. Yesu alisema katika Mtakatifu Yohana 5:24, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenituma Mimi, anao Uzima wa Milele na Milele," ule Zoe, Roho Mtakatifu, kwa sababu yeye aliamini. Kwa usahihi. Sasa, hadi wewe umpokee Huyo, wewe ni mwamini wa kujifanya, huyo aliye katika hilo kundi. Lakini wao wanapoamini kwa uhalisi, wakijitenga wenyewe, basi wewe unapojitenga mwenyewe mbali na kutokuamini kwako kote, na ukamwamini Mungu, unaenenda kwa udhabiti, ukichukua zile Amri, ukifanya kila kitu kilicho sahihi, basi Mungu atasema, "Kila ahadi katika kile Kitabu ni yako." Amina. "Zote ni zako! Fungua kwenye Hiyo, kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, yote ni yako!" Amina. "Kama mkikaa ndani Yangu na Neno Langu ndani yenu, mnaweza kuomba kile mtakacho, kitafanyika." Nini? Inakupasa ujitenge mwenyewe, kwanza, mbali na kutokuamini kwako.

61 Unasema, "Ndugu Branham, wewe unaliweka karibu mno."

Yesu alisema, "Katika siku za Nuhu kulikuweko na wanane waliookoka. Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana adamu."

"Hao ni wangapi, Ndugu Branham?" Huenda ikawa elfu nane, labda milioni nane, mimi sijui itakuwa wangapi. Lakini itakuwa katika uchache. Mmoja kutoka kwenye kila elfu mia moja, au kitu fulani kama hicho, ningesema. Vema.

62 Imani ya kisaikolojia, imani ya kiakili, pasipo uzoefu wa tendo halisi la kuzaliwa upya, msisimko, kanuni ya imani ya dini! Kama Roho Mtakatifu wa kweli aliye halisi yuko ndani pale, Yeye atalipokea hilo Neno; na hilo Neno litaishi kikamilifu tu kama Hilo lilivyosema lingeishi, kwa sababu ni Roho yule yule aliyenena Hilo, Yeye ananena Hilo kupitia wewe. Inapasa Hilo liwe hai. Hakika, liko hai. Siyo wewe unenaye, bali Baba akaaye ndani yako, Yeye Ndiye anayenena. Vema.

63 Abrahamu, mrithi wa vitu vyote.

Mimi, nilipojazwa kwa Roho Mtakatifu kama ninyi watu mlivyojazwa, nalipenda kutembea kote, na, kama jumba kuu lenye bidhaa za biashara, kila kitu pale ni changu. Mimi ni mrithi wa kila kitu chake. Na kama nilirithi jumba kuu lenye bidhaa za biashara, mimi-mimi ningependa kuona kile nilichopata. Mimi nilipofanyika kuwa Mkristo, nilitaka kujua kile nilicho nacho. Hivyo kama nilikuwa na jumba kuu lenye bidhaa za biashara, ningepita kote, na kuvuta droo na nione nini kilichoko ndani mle, na nitazame hapa na nione nini kilichoko ndani pale; kitu fulani kinaonekana kama kwamba kiko juu zaidi kule, nachukua ngazi na kukwea hadi kukifikia hicho. Ningefahamu hicho kilikuwa kitu gani. Kitu fulani kinaonekana kama kwamba siwezi kukikuta hapa, ninapiga magoti yangu na kuanza kuomba hadi nikifikie hicho. Hicho ni changu! Mungu aliahidi hilo. Uponyaji wa Kiungu, Nguvu za Mungu, miujiza yote hii na ishara na maajabu, Yeye aliahidi hilo.

Unasema, "Ndugu Branham, haya mambo yanatendaje kazi?" Kwa njia ya ahadi ya Mungu. Amina.

Uzao wa Abrahamu! Utukufu! Najisikia vizuri. Huenda naweza kuonekana mwendawazimu na kutenda kiwendawazimu, lakini niacheni tu peke yangu. Najisikia vizuri zaidi namna hii kuliko nilivyojisikia njia ile nyingine. Unaona?

64 Sura ya 14, tunamwendea Abrahamu, sasa tunaona kile kilichotukia katika sura ya 14. Wafalme walishuka kutokea sehemu mbalimbali za nchi, na walishirikiana na wafalme wa Sodoma, na wakaingia ndani na kuuchukua Sodoma, wakamchukua Lutu; ndugu yake aliyekuwa Abrahamu katika Bwana, wakamchukua na kumtoa nje, ndugu yake vuguvugu wa kidhehebu, na kuondoka na yeye. Sasa, kumbuka, Mungu alikuwa amemwambia tu Abrahamu kuwa kila kitu katika nchi kilikuwa chake.

"Na wanyenyekevu watairithi nchi." Unasema sisi tu wendawazimu? Wanakwenda kuimiliki nchi, kile kilicho juu ya nchi! Hakika, sisi ni warithi wa hilo.

Mtazame Shetani, Yesu alisema, "Kama Wewe utaanguka chini na kunisujudia mimi, nitakupa Wewe huu ulimwengu." Falme zote zinadhibitiwa na yule Mwovu, kila moja ya hizo. Yesu alisema hivyo. Biblia inanena hilo. Kila taifa na kila ufalme unadhibitiwa na yule Mwovu. Na Shetani alisema, "Mimi ninamiliki hizi. Hizi ni zangu. Nitakupa Wewe hizo kama Wewe utanisujudia mimi."

Yesu alijua kuwa Yeye alikuwa Mrithi wa hizo katika Utawala wa Miaka Elfu, hivyo Yeye alisema, "Rudi nyuma Yangu, Shetani." Yeye alijua kuwa Yeye alikuwa Mrithi kwa hilo.

65 Na leo wao wanazungumza juu ya watu walio wendawazimu wakimwabudu Bwana na wakiwa wanazaliwa upya. Wao wanaogopa jambo hilo la " kule kuzaliwa upya." Wao hawataki tu hilo wazo, nao walibadili Kitu Fulani kuwa badala ya hilo. Mmoja wao badala yake ameweka kushikana mikono; yule mwingine, kunyunyiza maji kidogo; yule mwingine, kutoa nje ulimi wake na kuchukua kipande cha mkate; yule mwingine, kucheza huko na huko sakafuni. Jambo lenyewe ni Kuzaliwa! Kama nilivyosema jioni ile nyingine, "Kuzaliwa ni mchafuko, mimi sijali huo uko wapi. Kama huo uko katika zizi la nguruwe au chumba cha hospitali, huo ni kuzaliwa, huo ni mchafuko." Na vivyo hivyo Kuzaliwa upya. Huo unakuraruararua kabisa, lakini kutokana na huo mchafuko Uzima mpya unakuja. Amina. Ndiyo.

66 Abrahamu alijua kuwa kila kitu kilikuwa chake, hivyo basi Lutu alipokuja ndani, yeye alisema, "Sasa subiri kidogo." Lutu alichukuliwa na mikono mikatili ya adui. Abrahamu alisema, "Huyo ni ndugu yangu, na nitakwenda kumtafuta." Sasa kumbuka, kulikuweko na takriban wafalme saba au wanane waliokwenda pamoja, na kuja chini na kuchukua kila kitu na kuondoka nacho. Nao walipotoka, Abrahamu aliwachukua watumishi wake na kwenda kumtafuta, ili kumrejesha ndugu yake aliyepotea. Huyo ni Mkristo halisi, alikwenda kumtafuta ndugu yake aliyepotea! Je, Abrahamu alifanya nini wakati alipompata? Yeye aliwaua hao wafalme; na kurudi, akimleta ndugu yake, baada ya mapambano.

67 Tazama, kulikuweko na Mfalme mmoja aliyekuja kumlaki na Abrahamu, akiwa anarudi, Melkizedeki. Melkizedeki, Yeye alikuwa nani? Yeye hakuwa na baba, Yeye hakuwa na mama. Kamwe Yeye hakuzaliwa, kamwe Yeye hafi. Hana baba, hana mama, hana mwanzo wa siku wala mwisho wa uhai. (Haikuwa Mwana wa Mungu; kwa sababu Yeye alikuwa na Baba na mama, wote wawili walizaliwa na kufa, na kufufuka tena.) Lakini huyu Mtu kamwe hakuwa na baba au mama, Yeye ni Mungu! Hakika, Hicho ndicho Kitu pekee kilicho cha Milele na Milele.

Na Yeye alikutana na Abrahamu baada ya vita kwisha, akionyesha hilo kwa Uzao wa Abrahamu; baada ya sisi kumwendea ndugu yetu aliyeanguka, na vita kwisha. Melkizedeki aliandaa chakula gani? Divai na mkate, ushirika. Amina. Vita vinapomalizika, ndugu! Aliporudi, akimleta ndugu yake aliyepotea arudi nyumbani tena, akimrejesha tena. Na vita vilipomalizika, Melkizedeki alimlaki na kumpa ushirika wa meza ya Bwana. Yesu alisema, "Mimi sitakula au kunywa tunda la mzabibu tena hadi nitakapokula mpya pamoja nanyi katika Ufalme wa Baba Yangu." Ndiyo, bwana. Sasa vita vilikuwa vimemalizika, Abrahamu alikuwa amerejea, ile sura ya 14; na yule Mshindi alikutana naye, yeye alipokuwa akiingia ndani pamoja na yule Mshindi.

68 Mwanzo 15 sasa, kabla hatujafunga, kwa sababu ni wakati wa kufunga sasa. Sikiliza jambo moja zaidi kabla hatujaondoka.

Na itanibidi kulichukua hilo kesho jioni tena, kwa sababu bado sijafikia tu somo langu, bado kufikia mahali pangu, juu ya Yehova-Yire. Nataka nilifikishe chini pale, kama Bwana akipenda.

Sasa penye sura ya 15, ninalo hapa kuwa agano lilithibitishwa kwa Abrahamu, uthibitisho wa agano. Katika maneno mengine, ni wakati Mungu alipoapa, na Mungu alipoweka ahadi na kuthibitisha hiyo ahadi kwa Abrahamu. Katika sura ya 15, tunaona kuwa, uthibitisho wa kile kiapo Mungu alichosema.

Abrahamu alimwambia Mungu, "Mrithi wa nyumba yangu bado ni huyu Eliezeri wa Dameski."

Na Yeye akamwambia Abrahamu, "Lakini huyo siyo mrithi wako, kwani ni

atakayetoka kwenye viuno vyako ndiye mrithi wako." Na Yeye alimwahidi Abrahamu.

Abrahamu akasema, "Mimi nitajuaje hili?"

69 Ee, sasa, ndugu, hapa kuna jambo litakalokuamsha! Mtazame Mungu. Yeye alisema, "Nenda ukaniletee mbuzi jike wa umri wa miaka mitatu, na ng'ombe jike, wa umri wa miaka mitatu, na kondoo dume wa umri wa miaka mitatu." Na Abrahamu akawachukua hao, na njiwa wawili…njiwa na hua."

Sasa, njiwa na hua walikuwa na uwakilishaji; hawa wanyama wenye umri wa miaka mitatu, na walikuweko watatu. Sasa Yeye anakwenda kufanya agano, kuthibitisha agano. Sasa sikiliza kwa makini, hilo lisikupite. Na ndipo tutalichukua kesho jioni wakati Yeye anapokutana na Abrahamu hapa tena, Bwana akipenda. Tazama.

Sasa Yeye alisema, "Niletee ndama wa umri wa miaka mitatu, mbuzi jike wa umri wa miaka mitatu, na kondoo dume wa umri wa miaka mitatu, njiwa, na hua."

Na Abrahamu alikwenda na kuwachukua hao wanyama, na kuwakata vipande viwili viwili na kuwaweka, kipande kwa kipande; lakini hua na njiwa, yeye hakuwatenga hua na njiwa. Hua na njiwa ni jamaa moja. Hivyo hilo liliwakilisha uponyaji wa Kiungu, ambao katika maagano mawili ni kwa imani, unaona, wao waliponywa; mmoja tu kwa mwingine, yule mwingine. Kama agano la kale lilikuwa na uponyaji wa Kiungu ndani yake, ni kiasi gani zaidi Hili litakuwa nao! Unaona, kama dhabihu ya kale ilikuwa na uponyaji, vipi juu ya Hii ambayo ni bora zaidi! Unaona?

70 Sasa, lakini angalia kile yeye alichofanya hapa. Yeye alichukua hawa wanyama watatu na kuwakata vipande viwili viwili, na kuwaweka, kipande baada ya kipande. Na ndipo Abrahamu aliporudi. Sasa, hiyo ilikuwa dhabihu. Na yeye alitazama hadi jua likawa linazama. Na ndege wakashuka chini kutoka angani, juu ya dhabihu ya Abrahamu, ndege wala mizoga. Na Abrahamu akawafukuza, akawatisha kuwafukuza waondoke.

Huu ni mfano wa nini? Uzao wa Abrahamu katika siku ya mwisho, ukifukuza mapepo kutoka kwenye Dhabihu, ukiyafukuza mbali na ile Dhabihu. Mungu aliahidi hilo, hiyo Dhabihu, Kristo, yule yule jana, leo, milele, na hizo zote roho zisizoamini zikijaribu kuila na kuimaliza Hiyo. Huyo mtu wa Mungu, Uzao wa Abrahamu, unasimama pale ukifukuza mapepo, mbali na Hiyo! Akithibitisha lile agano sasa, ule uthibitisho, ikionyesha kuwa Uzao wa Abrahamu katika… Namaanisha Uzao mtiifu wa kifalme. Kumbuka, ule uzao wa asili ulishindwa, kwa sababu ulipokea sheria badala ya Neno la neema. Na hivyo ilivyokuwa katika huu "uzururaji," katika Mataifa katika siku ya mwisho. Lakini kuna Uzao, Uzao wa kifalme wenye Neno, unaosimama katika ukweli, ukifukuza mapepo, ukifanya ishara kuu na maajabu, ukiondoa kutokuamini kote na kuuweka mbali na Neno, ukiidumisha Dhabihu kuwa safi, ukidumisha Neno kuwa takatifu, Neno likidumu kuheshimiwa; siyo kuweka kitu chochote pamoja Nalo, kuongeza lolote kwenye Hilo; ukiliweka Hilo mahali Pake lenyewe, ukilinda, pasipo kuruhusu chochote kuligusa Hilo.

71 Sasa angalia, ukaja usingizi mnono juu ya Abrahamu, mauti. Na baada ya usingizi mnono, yeye aliona tanuru la moto, ambalo ni kuzimu, likitoa moshi, kuwa kila mwenye dhambi anapaswa kwenda huko. Lakini mbele pale kulitokea Nuru ndogo nyeupe. Tazama hiyo Nuru ndogo nyeupe, ilikwenda katikati na ilitenganisha zile dhabihu, ikaenda katikati yake, Mungu akithibitisha kuwa ambacho Yeye angelifanya kupitia Uzao wa Abrahamu.

Sasa, Wayahudi siku zote waliamini Mungu alikuwa Mmoja. Na Mungu ni Mmoja. Lakini Yeye alikuwa anaonyesha hapa, kwa hizi dhabihu tatu zilizo safi, kwamba utatu wa Mungu ungeliwakilishwa katika Mmoja katika Uungu kimwili.

72 Sasa angalia katika siku za kale, katika siku za watu wa mashariki, agano lilipofanyika, hivi ndivyo wao walivyofanya hilo. Kama, tunakuja na tunamwua mnyama, tunamgawanya huyo mnyama katika vipande viwili, na tunasimama katikati ya huyo mnyama, na pale tuliandika agano. Sasa katika China…

Jinsi katika Japan, wanapofanya agano, wanachukua chumvi kiasi fulani nao wanasimama na kuweka ahadi yao, nao wanatupiana chumvi wao kwa wao. Hivyo ndivyo wanavyofanya katika Japan, wanafanya agano, wanatupa chumvi. Chumvi inatia ladha, unaona. Nao wanatupiana chumvi wao kwa wao, hilo ni-hilo ni agano.

Sasa katika Amerika, jinsi tunavyofanya agano, tunatoka nje na kuwa na kitu cha kula, na kushikana mikono, "Nipe mkono wako, jamani. Je, tumekubalina?" "Tumekubaliana." Hilo ni agano.

73 Lakini katika nyakati za kale, katika wakati wa Abrahamu, jinsi wao walivyofanya agano ilikuwa kuua dhabihu, na kusimama katikati ya hii dhabihu; na ndipo, walipofanya, wao waliandika agano juu ya kipande cha ngozi ya mwanakondoo, halafu wanakichana hicho. [Ndugu Branham anachana kipande cha karatasi, na kutoa kielelezo-Mh.] Mmoja alichukua kipande kimoja, na mmoja akachukua hicho kingine. Sasa wakati hili agano lilipothibitishwa na kuletwa pamoja, hapakuwepo na mmoja ambaye aliweza kuigiza hilo. Unaona, inapasa liungane na kuumana, herufi kwa herufi, kabisa tu jinsi hilo lilivyokuwa. Hilo linaonyesha kuwa mmiliki sahihi wa hiki kipande ana sehemu, hili ni agano lile lile, ambalo inapasa liunganike pamoja na kulingana tu kabisa hivyo hivyo.

74 Na Mungu alikuwa anaonyesha pale kwa Abrahamu, kuwa kupitia Uzao wake, kwamba Mungu Mwenyewe angelifanyika mwili na ndipo impase Yeye atenganishwe vipande pale Kalvari; ambapo Kristo, akiwa Mungu duniani, Yeye alitenganishwa vipande. Mungu alimchanachana Yeye vipande, ule Uzao wa kifalme wa Abrahamu, na kutoa Uzima ndani Yake; na kuufufua ule Mwili, akapaa juu na kuketi kwenye Kiti Chake cha Enzi Mbinguni; na kutuma Roho Wake juu ya Kanisa, kwamba Kanisa ilipasa liwe na yule yuleyule yule Roho aliyekuwa ndani ya Kristo ili kufanya hilo liungane pamoja, likimfanya Kristo yule yule jana, leo na hata milele! Uthibitisho wa agano, Mungu akilithibitisha agano. Mungu akitenganisha, akichanachana Uzima kutoka kwa Kristo, Mwana Wake, akichukua Roho kutoka Kwake; kama Yeye alivyokatakata hawa wanyama vipande viwili, akisimama katikati ya hao wanyama. Ile Nuru, Mungu Mwenyewe, alitembea katikati yao, akionyesha kuwa Yeye alitenganisha ule Mwili: ule Uzao, Uzao wa kifalme; na kuchukua Roho na kuituma Hiyo juu ya Kanisa. Na Kanisa la leo linalokwenda kukutana na Kristo, italipasa kuwa na Roho yule yule ambaye Yeye alikuwa naye, kwa sababu hiyo itapasa iwe Herufi kwa Herufi, Neno kwa Neno. Na Yeye ndiye Neno! Yesu alisema, "Yeye" (kiwakilishi binafsi) "aniaminiye Mimi, matendo yale niyatendayo Mimi, naye atayatenda pia." Akilithibitisha lile agano, ule Uzima ulio ndani ya Kristo utakuwa ndani ya Kanisa, ule Uzao wa kifalme wa Abrahamu.

75 Subirini kwa kitambo kidogo, ndugu, juu ya Pentekoste. Wao walikuwa orofani…Kama wewe ungewahi kuwa pale na kuona mchoro halisi, jinsi ulivyochorwa, wao walikwenda kupita ngazi upande wa nje na kwenda juu orofani. Wao walikuwa na mishumaa midogo ya mafuta ya mzeituni ikiwaka. Wao walikuwa juu pale kwa siku kumi mchana na usiku, milango yote ikiwa imefungwa. "Kukaja ghafla kutoka Mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wenye nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Ndimi kama moto, ndimi zilizogawanyika za moto, ulikaa juu ya kila mmoja wao. Wote walijazwa Roho Mtakatifu, wakatoka wakaenda uani, wakinena kwa lugha nyingine."

Angalia, huu Moto uliogawanyika ulikuwa nini? Ulikuwa Nguzo ya Moto, Roho Mtakatifu, Mungu, yule Malaika aliyewaongoza wao kupita jangwani, Yule ambaye alidhihirishwa mbele zao. Mungu alikuwa amejikata vipande Mwenyewe na kujigawanya Mwenyewe miongoni mwa watu, Roho Mtakatifu, na kwa pamoja sisi tunakuwa Kanisa la Mungu aliye hai. Agano! "Abrahamu na Uzao wake baada ya yeye, ule Uzao wa kifalme." Ule ule Uzima uliokuwa ndani ya Kristo, ndani ya Kanisa, ukitenda matendo yale yale ambayo Kristo aliyatenda. Amina. Ni kitu kizuri iliyoje, marafiki!

76 Ndiyo tu wakati, inanipasa tu nifunge hili. Ndiyo, nakwenda kuchelewa kupita kiasi. Nita-nita…Je, hilo litakuwa sawa kama nikilichukua hili kesho jioni kuanzia papa hapa? Nataka sana nifikie Yehova-Yire. Lakini nataka ninyi muone hilo kile lilicho, kwamba hicho kitu cha kudai kuwa u Mkristo, ndugu, ni wakati wa kanisa kupata kwamba…Kama Mungu alifanya hizi ahadi, hizo ni kweli. Ni lazima zitukie.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa kitambo kidogo tu. Hili ni kali na gumu. Hilo linachoma. Mimi sipendi kufanya hilo. Huyu mhudumu aliniambia, yeye alisema, "Ndugu Branham, mbona fulani na fulani, wewe unafanya hilo?"

Mimi nikasema, "Mimi sina vipindi vya televisheni vya kudhaminiwa, redio. Mimi huwa nakwenda tu namna hii, ambapo ninaweza kwenda kokote." Nikasema, "Ni nani anayekwenda kuwaambia hao? Inapasa kuwepo na sauti mahali fulani inayosema hilo."

77 Sasa Mungu yuko hapa, marafiki. Na kama umejiita mwenyewe wewe ni ule Uzao wa Abrahamu, na kufikiri kuwa wewe…Sasa usi-…Sikiliza, ni nafsi yako, rafiki. Ni nafsi yako. Usibahatishe juu ya hili, kwani jioni hii yaweza kuwa wakati wako wa mwisho unaopata nafasi ya kufanya hili. Kama unaonea haya maisha yako, ukijiita mwenyewe mtoto wa Mungu, na unaishi jinsi ambayo umekuwa ukiishi; na unaamini kwamba Neno la Mungu ni ukweli, na wewe una makosa, nataka wewe uombe tu kwa kitambo kidogo, mwombe Mungu achunguze maisha yako. Omba tu.

78 Baba wa Mbinguni, hii ingeweza kuwa jioni ya mwisho kwa wengi wetu. Tunafikiri, nyakati chache za jioni zilizopita katika Los Angeles, mwanamke mzee wa umri wa miaka sabini akiwa ameketi pale, na yeye alitembea hadi madhabahuni na kutoa maisha yake kwa Kristo. Jioni ile yeye alikufa kitandani. Neema ya Mungu, ile saa ya mwisho. Baada ya kuishi miaka yote ile pasipo kumjua Yeye, ndipo ukamwita yeye penye saa ya mwisho. Neema ya ajabu.

Baba Mungu, zungumza na mioyo hapa jioni hii. Wewe unajua kusudio la hili. Wewe unajua, Baba, inapa-inapasa ifikie wakati kwamba jambo fulani inabidi lifanyike. Sisi-sisi tunaona hiyo hali, na jinsi kadiri inavyokuwa mbaya zaidi wakati wote. Nasi tunatambua kuwa kipindi cha kanisa la Pentekoste, katika siku za mwisho, ni Kipindi cha Kanisa la Laodikia, kilicho pekee ambacho Kristo alitolewa nje ya kanisa, akisimama, akibisha hodi akijaribu kurejea ndani. Ee Mungu, turehemu.

79 Na kama nilivyowakaripia dada zetu jioni hii, Bwana, hebu wao wajue kuwa nyuma kule hapo mwanzo, hilo lilipoanza, ilikuwa ni Hawa. Na hilo lipo hapa tena. Injili ilikuja ndani kwa njia ya Neno, na jinsi kwamba yeye alitenda kile yeye alichotenda (na tazama leo) kwa kutoa hoja; mtazame mama yake, kile yeye alichowaza jinsi alivyokuwa tofauti, Biblia ile ile.

Mungu, ndugu zetu, kama ambavyo imenipasa kuzungumza nao kwa ukali, Bwana. Nina uchu, nina-nina-ninawapenda wao. Wewe unajua ninawependa, Bwana. Mimi-mimi-mimi nimeweka miaka thelathini na moja hapa kwa ajili yao, na Wewe umethibitisha Neno Lako, na kila kitu kingine. Bwana, mimi sijui kitu kingine cha kufanya. Lakini ninapoona kanisa ninalolipenda, kanisa la Kipentekoste, lile lililosimama nyuma yangu na kunisaidia; Mungu, ni upendo wa Kikristo uliokufanya Bwana kuondoa uovu mbali na hilo. Ni upendo unaokufanya Wewe ufanye hilo, Baba. Wewe unajua ni huo. Na najaribu kuwaambia hao watu, "Msijaribu kutoka nje pale, mkifanya haya mambo." Vile-vile vizuizi vimeshateremshwa, na tumeanguliwa kupitia kanuni zetu mbalimbali za imani ya dini na vile vitu tulivyovileta katika kanisa, na kuondokana na siku za miujiza, tukienda mbali na uponyaji wa Kiungu, tuondokana na ile-ile njia ambayo watu wanapaswa kutenda na kuvaa.

80 Na Wewe ulifanya agano na Adamu, na moja kwa Hawa; uliweka agano tofauti, na tofauti kwa pamoja, na kusema ilikuwa ni makosa kwa mwanamke kutenda kama mwanamume. Yeye angelikuwa na hali ya kike. Yeye mwanamke angepaswa kuwa wa hali ya kike siyo ya kiume. Na leo yeye mwanamke anajaribu kujiweka katika hali ya kiume; mwanamume, hali wewe ni wa kike.

Bwana, na-na hili papa hapa penye siku za mwisho, hapa hapa penye Pwani ya Magharibi, papa hapa kwenye mwisho wa ustaarabu, tunamkuta mwanamke akifanya uharibifu kabisa kama wao walivyofanya hapo kwanza. Na ndilo hili hapa, liko miongoni mwa dada zetu. Ee Mungu, kwamba hilo linavunja tu moyo wangu, Bwana. Na najua kama hilo linanifanya mimi (mwenye dhambi) nijisikie hivyo, hilo linafanya nini Kwako, kwa kuona jinsi hilo limefanyika kuwa mungu mke. Na hili Hollywood ya ajabu inayovutia dhambi! Na ilikuwa ni makosa kwa wao kwenda kwenye maonyesho ya picha, ndipo yule Mwovu akalitupia hilo moja kwa moja ndani ya nyumba yao, na-na aina zote za vipindi visivyohakikiwa, na uchafu barabarani.

Na, Ewe Mungu, ni-ni wakati wa ukichaa. Ni wakati wa kuchanganyikiwa akili. Ni-ni wakati ambapo mwanadamu hatasimama na kusikiliza, na kuchunguza. Na chini ya misisimko, na kadhalika, wao bado hudai kuwa wewe ni Uzao wa Abrahamu. Mungu, jinsi Wewe ulivyosema hilo lingekuwa, maroho yatakuwa karibu mno katika siku za mwisho, pamoja na uigizaji, hadi karibia hilo lingewadanganya wateule, kama ingaliwezekana. Na hilo liko hapa. Mungu, usiruhusu hawa watu, usiruhusu mmoja afanye hilo. Tafadhali, Baba. Naomba kwa ajili yao, kila mmoja. Katika Jina la Bwana Yesu, tujalie hilo.

81 Sasa tunapokuwa tumeinamisha vichwa vyetu. Ningefanya lolote kwa ajili yenu. Na kama nawapigia watu kelele ili tu kuwa mkatili, Mungu kamwe asingekuwa pamoja na mimi; mimi sistahili kuwa hapa, nastahili kuwa nje kule mahali fulani nikipasua kuni au kitu fulani. Lakini, marafiki, huo-huo ni ukweli, lichunguze hilo na uone kama haliko katika Andiko. Na hilo linapaswa kufunuliwa katika hii siku ya mwisho.

Sasa ninyi ni waaminifu vya kutosha? Je, uko hasa chini ya hilo kokwa la nje, je, kuna kitu fulani kilicho halisi juu yako, ambacho unakusudia kukiri kuwa una makosa? Wakati kila kichwa kikiwa kimeinamishwa, kila moyo, na kujiweka wakfu kwa uaminifu mno, je, utainua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham. Mimi nina makosa. Kwa neema ya Mungu ninakwenda kurekebisha"? Mungu akubariki, wewe, wewe, wewe. Hilo ni sawa, inua juu mkono wako, Yeye anauona huo. Katika sehemu ya orofani, Mungu anakuona. Inueni mikono yenu. Wewe, na wewe-wewe…Ndilo hilo.

82 Sasa hapa kuna baadhi yenu ninyi wanawake mlioketi hapa mkiwa na nywele fupi, na hamkuinua mikono yenu juu. Mna tatizo gani? Ninyi mna makosa! Usijaribu kukutana na Mungu ukiwa hivyo. Utahukumiwa kwa hakika kama nilivyosimama katika hii mimbara. Unamaanisha kanisa la Kipentekoste limefikia katika sura kama hii ambayo lime-lime-limekufa ganzi hadi linaona aibu kukiri jambo hilo kuwa ni makosa? Usifanye hilo. Mungu akureremu.

Mimi naamini. Uwe na imani. Hebu nisubiri tena. Mungu akubariki wewe pale, mpenzi. Mungu akubariki, dada. Hilo ni zuri. Weka…Yule…Mungu akubariki. Hilo ni sawa. Unaweza kukubali hilo sasa; huenda asubuhi ikawa umechelewa mno, saa moja tangu sasa huenda ukawa umechelewa mno. Mungu akubariki. Huo ni uaminifu. Mungu akubariki. Sema, "Mimi nina makosa." Inahitaji mtu halisi ili kukubali wanayo makosa. Hicho ni kitu fulani kilicho halisi. Mungu akubariki, bibiye. Mungu akubariki, bibiye. Mungu akubariki. Hilo ni sawa. Ndiyo, endelea tu kuomba. Mungu akubariki. Kama nikishindwa kuona mkono wako, Yeye hashindwi. Yeye anajua kila wazo lililoko katika akili yako. Hilo ni sahihi kabisa. Mungu akubariki, naona mkono wako. Hilo ni zuri. Mungu akubariki, bibiye kijana. Mungu akubariki, dada. Hilo ni zuri.

Mungu akubariki wewe pale, bibiye kijana. Ndiyo, kurudi kwa njia za maisha. Kabla haya mambo ya kale hayajaupiga ganzi moyo wako wa ujana, mgeukie Mungu sasa, mpenzi. Hilo ni sahihi, ufanye hilo. Ninaye binti mdogo pale takriban wa umri wako. Mungu akubariki, mpenzi. Mungu akubariki. Ndiyo, Mungu akubariki, dada.

83 Vipi kuhusu wewe, ndugu? Uone aibu, unamruhusu mke wako anatenda namna hiyo na kuvaa kaptula, na kuvaa namna hiyo na kwenda barabarani. Unajiita mwenyewe mwana wa Mungu? Je, hujionei aibu mwenyewe? Mungu akubariki. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Hilo ni sahihi, kubali kuwa una makosa. Naam. Kama wewe…

"Yeye azifichaye dhambi zake hatafanikiwa; yeye atubuye dhambi zake atapata rehema." Mungu akubariki. Yeyote zaidi? Nyuma katika roshani, juu pale roshani. Yeye anakuona wewe juu pale. Yeye anajua kila wazo lililoko katika moyo wako.

Sasa inueni vichwa vyenu kwa dakika moja.

Nasema kuna takriban hamsini au sitini katika chumba hiki walioinua juu mikono yao, vijana na wazee. Asante. Huyo ni bibiye halisi na mwanamume mwungwana. Nawathamini. Kuna-kuna matumaini kwenu mnapotaka kukubali kuwa mna makosa.

84 Kabla sijafanya wito wa madhabahuni, nakwenda kuomba kwa ajili ya hizi leso.

Baba wa Mbinguni, hizi leso zinawakilisha watu walio wagonjwa, akina mama na akina baba wanaosubiri, watoto. Wakati mmoja, tunafundishwa katika Biblia, kuwa wao walichukua leso na aproni kutoka kwenye mwili wa Mtakatifu Paulo. Watu walimwona yeye, walijua kuwa Roho wa Mungu alikuwa juu yake. Paulo alikumbuka kwamba Elisha alimwambia yule mwanamke wa Shunami, yule aliyemwambia Gehazi, "Chukua hiki kitu na uende ukiweke juu ya mtoto." Yeye alijua kuwa kile yeye alichogusa kilibarikiwa. Paulo, wao walichukua leso na aproni kutoka mwilini mwake, na maroho machafu yakawatoka watu, magonjwa yakaondoka. Sasa, Bwana, sisi siyo Mtakatifu Paulo, lakini Wewe bado ni Mungu, Mungu yule yule.

Siku moja Israeli lilikuwa njiani mwake katika kuwajibika, likienda kwenye nchi ya ahadi. Na kitu fulani kikawa kimewatenga na ile nchi ya ahadi, Bahari ya Shamu. Mwandishi mmoja alisema, "Mungu alitazama chini kupitia ile Nguzo ya Moto, akiwa na macho yenye hasira, na bahari ikaogopa, na ikaviringisha kuta zake na kufungua njia

kavu kwa ajili ya Israeli ili wavuke kwenda nchi ya ahadi."

Mungu, wakati hizi leso zinapopelekwa kwa wagonjwa na wanaoteseka, hebu Mungu wa Mbinguni atazame chini kupitia Damu ya Mwana Wake Mwenyewe, na hebu yule Mwovu, anayewashikilia hao watu wagonjwa, aogope na kuondoka wakati hizi leso za ishara za huu mkutano jioni hii, ambapo Neno na ile Kweli imeletwa ili kutimia; wagonjwa na wanaoteseka wafanyike kuwa wazima; mioyo iliyovunjika, na kwenda chini kwenye nyumba ya kuhifadhia maiti katika dakika chache; tujalie kwamba yule Mwovu ataondoka, na watu watavuka kule katika nchi ya afya nzuri Mungu aliyowaahidi wao. Natuma hizi leso, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya kusudi hilo. Amina.

85 Na Mungu anajua moyo wako. Yeye anajua hali yako. Ili tu kuonyesha; na hebu niwaambie, kuna kundi kuu la watu ndani hapa ambalo halikuinua mkono wao, linalopaswa kuwa lingeinua huo. Sasa, kama nikikuita moja kwa moja kutokea kwenye hili jukwaa, niseme wewe ulikuwa nani, hilo litaumiza hisia za mtu fulani. Sasa, mmeniona mimi nikifanya hilo mara nyingi. Niliona, Yesu alisema, "Yaache magugu na ngano vikue pamoja. Malaika watakuja na kufunga makapi na kuyateketeza, kwanza."

Na huu ni wakati wa kufunga. Kila mmoja wao anayekwenda katika shirikisho la makanisa, madhehebu yote. Hilo ni sahihi. Hilo ni sahihi. Muunguno wa Ulimwengu, Baraza la Makanisa, kila dhehebu likijivuta na kuingia moja kwa moja ndani yake, hicho kitu kikubwa kikiendelea. Wote wakirejea kwa Rumi kama tu wao walivyoahidi, "sanamu iliyofanyika kuwa mnyama," nguvu, shirikisho la makanisa, kile tu hasa Mungu alichosema kingetukia. Wao hao hapo, wakikuacha uende, na wakikuambia hilo ni sawa kufanya hili, na wanaogopa kusema chochote juu ya hilo, wanaogopa hilo lingevunja tikiti ya chakula mahali fulani.

86 Hebu nikuambie jambo fulani, ndugu yangu, dada, Mungu anakufunulia wewe kuwa nakupenda. Siyo kutofautiana; ni kuwa mkweli. Usibahatishe. Usingeweza kuvuka taa nyekundu, kwa sababu ya mwili wako. Vipi kuuhusu nafsi yako? Usivuke mojawapo ya taa nyekundu za Mungu.

Baadhi yenu ni wagonjwa. Amini kwa moyo wako wote. Mtu fulani aliyekata tamaa katika jambo fulani, uwe tu na imani. Nitakuonyesha kama Yeye kwa kweli, kama hiyo ni ile Kweli au la. Abrahamu, unakumbuka Malaika alikuja kwake na Yeye Bwana alifanya nini? Ona kama hilo ni jambo lile lile.

87 Hapa kuna bibiye kijana akiwa ameketi papa hapa, papa hapa, yeye ana saratani. Yeye ana kivimbe, na yeye anaendea upasuaji. Yeye ananitazama sasa, na hizo shanga nyekundu shingoni mwake. Wewe unatokea Portland. Lakini kama utaninii…Kama hilo ni sahihi, inua juu mkono wako. Hilo ni sahihi. Unaona? Mimi sikujui wewe, sisi ni wageni mmoja kwa mwingine. Lakini hilo ni kweli. Sasa wewe unawezaje kuketi pale, ukiwa na imani ya kutosha kugusa vazi la Kristo wakati huyo Malaika wa Nuru alipokuja juu yako namna hiyo, neema ya Mungu? Likubali Hilo, bibiye. Amini Hilo. Siyo tu hilo, lakini amini Injili yote.

Hapa ameketi mwanamke akiwa ameketi papa hapa nyuma. Tazama hapa, bibiye. Unaumwa na tatizo la utumbo mkubwa. Amini kwa moyo wako wote. Ndiyo, wewe ni mgeni kwangu. Amini kwa moyo wako wote, na uwe mzima.

88 Kuna mwanamume aliyeketi kando yako, inampasa yeye aende nyumbani. Yeye hawezi kukaa zaidi. Yeye ana tatizo na masikio yake. Yeye ana tatizo la…Yeye ana mafua, na yalisababisha kukohoa. Yeye hawezi kuondokana na hilo, hiyo ni-hiyo ni namna ya msongamano wa matatizo mengi yaliyoko ndani. Hilo ni sahihi, bwana. Wewe unafanya kazi kwenye aina fulani ya kiwanda kama kombora au kitu fulani kama hicho. Inakupasa urudi kazini kwako. Mimi ni mgeni kwako. Kama hayo mambo ni kweli, inua juu mkono wako. Vema. Kama unayo imani ya kutosha kumgusa Bwana Yesu, kwa nini usiwe mwanamume halisi na uamini hilo kwa moyo wako wote?

Kuna bibiye aliyeketi nyuma kule, yeye ana aina fulani ya ugonjwa wa ngozi mikononi mwake. Yeye hata hajui ni kitu gani. Daktari hata hajui ni kitu gani. Yeye amekuwa nao kwa miaka na miaka. Ee, yeye anakwenda kulikosa hilo, kwa hakika tu kama ulimwengu. Bibi Daniels, McDaniel. Hilo ndilo jambo lote lenyewe. Ida McDaniels, amini kwa moyo wako wote. Mimi simjui yule mwanamke, kamwe sikuwahi kumwona yeye. Lakini pale kuna ile Nuru juu yake.

89 Ni kitu gani? Yeye anakujua wewe! Na Yeye anajua kuwa wewe una makosa!

Mungu yule yule anayenena kupitia mimi namna hii, ananena kupitia mimi kupitia Neno.

Sasa, kila mmoja ndani hapa anayetambua Uwepo wa Mungu, na unajua kuwa umekosea, hebu tuje madhababuni sasa. Njooni juu hapa kwa dakika moja tu, hebu mimi niombe kwa ajili yenu. Kama wewe unajua umekuwa makosani, unataka kukiri kuwa uko makosani. Unataka kuwa Mkristo halisi tangu sasa na kuendelea, njoo juu hapa kwenye madhabahu. Mimi sitaki tu kuita jina lako, hali-halingekuwa la Kikristo. Juu ya kibaraza, njoo kuteremka chini, hii ni nafasi yako. Njoo hima hapa chini sasa! Njoo madhabahuni, useme, "Nakuja, Bwana." Mwenye dhambi, tengeneza njia yako kuelekea madhabahuni, huenda hii ikawa nafasi yako ya mwisho. Je, hutakuja sasa tunapo…kinanda kinapiga vizuri, "Ninakuja, Bwana, nakuja sasa Kwako." Vema, kila mtu aimbe sasa.

> Nakuja, Bwana!
> Nakuja sasa Kwako!

90 Je, hutakuja? Shuka chini kutoka roshani, shuka chini. Njoo juu. Vipi kuhusu ninyi, ninyi watu mnaokiri kuwa Wakristo. Uzao wa Abrahamu? Mungu awabariki, wanawake. Mungu awabariki, dada zangu. Ndiyo. Kwa hakika Mungu ataliheshimu hilo. Ninyi ni wakweli. Huenda mchungaji wako ameshindwa kukuambia wewe hilo. Nenda nyumbani na uchukue Biblia yako, na uone kama hilo ni sahihi, au la. Unajua hilo ni sahihi, kabla hata mimi sijasema lolote. Ninyi wanawake wa kipentekoste, msingejipamba kwa ajili ya chochote. Hakuna chochote katika Biblia juu ya mapambo; Yezebeli pekee, yeye alipamba uso wake na vitu, kwa rangi na vitu. Lakini kuna katika Biblia juu ya ninyi kuvaa nywele ndefu, "Ni kitu kisicho cha kawaida kwa mwanamke hata kuomba akiwa na nywele zilizofupishwa, kukata nywele."

> …Kwako!

Unataka kuwa sahihi na Mungu, katika Uwepo wakati Yeye Mungu akiwa hapa? Njoo! Simama wima, weka msimamo kwa ajili Yake! Simama kwa miguu yako na uje chini, useme, "Nakuja. Na-nakwenda kufanya onyesho.

Nataka ulimwengu wote ujue kuwa mimi nina makosa, na nataka niwe sahihi mbele za Mungu." Njoo sasa!

> Nakuja, Bwana!
> Nakuja sasa Kwako!
> Nioshe, nitakase katika Damu
> Ile iliyotiririka kutoka Kalvari.

Tena, kila mtu!

> Nakuja…Njoo… (Kuna wengi nje kule, kumbuka.
> Ndiyo, hilo ni sahihi.)
> …mimi, nitakase katika Damu Yako
> Ile iliyotiririka kutoka Kalvari.

91 Kuna watu bado wanakuja, endeleeni tu kuomba. Sasa, marafiki, mimi sishawishi sana. Naamini Neno hufanya kazi Yake wakati linapotoka nje huko. Usimhuzunishe Roho Mtakatifu. Huenda ikawa ni nafasi ya mwisho utakayowahi kuwa nayo; natumaini sivyo. Je, wewe unajua hilo linafanya nini kuona wewe ukikubali una makosa? Hilo linaniambia kwa kuna kitu fulani kilicho halisi pale, ambacho kwa kweli unataka kufanya kiwe sahihi. Sasa pamoja na kinanda tu, kwa taratibu kama utaweza, inapozungumza. Njooni hima, watu, njooni tu moja kwa moja. Nataka muendelee kuja. Je, mnajua kile hawa watu walichofanya? Wengi wa hawa ni washirika waanzilishi wa kanisa, nao wanajua mimi nimesema ile Kweli.

Siyo mimi. Kama tu wakati Musa alipokwenda chini kule ili kuwaambia wale watu juu ya Bwana; na Bwana, chini ya Nguzo ya Moto, alilithibitisha Neno na kuonyesha kuwa Hilo lilikuwa sahihi. Ile ile Nguzo ya Moto iko papa hapa pamoja nasi. Ni Kristo yule yule, akitenda kitu kile kile kwa ajili ya kipindi cha Mataifa, kama Yeye alivyoahidi kufanya.

92 Hilo linanifanya mimi niamini nini? Kuwa wewe ni halisi katika moyo wako. Nini kilichokufanya usimame kwa miguu yako? Kwa sababu Kitu Fulani kilichokuwa mahali hapo, kile kilichosema, "Wewe umekosa." Sasa huyo alikuwa Mungu, kwa sababu baadhi yenu mnaojihisi kufedheheshwa kusimama hapa namna hiyo mbele za watu, baada ya

kuungama. Lakini hilo linaonyesha kuwa hiki Kitu Fulani halisi Hicho kilichosema, "Una makosa," na Hicho kilikuja na Neno, kupitia utambuzi. Kupitia…

Hizi karama zilitumwa kwa kanisa kwa ajili ya nini? Karama ya kwanza ni ipi? Kitu cha kwanza ni kipi? Mitume (ambao ni mmishenari), manabii, walimu, wachungaji, wainjilisti. Wote kwa pamoja ni kwa ajili ya kulikamilisha Kanisa.

93 Na Neno la Bwana linakuja wapi, kwa nani? Neno la Bwana huja kwa nabii, siku zote, halihojiwi. Siyo karama ya unabii; karama ya unabii iko kwa mmoja, na ndipo kwa mwingine. Nabii huzaliwa, aliwekwa na Mungu tangu asili. Yesu Kristo alikuwa Mwana wa Mungu, Mwana wa Mungu aliyejulikana tangu asili. Isaya alimwambia Yohana, Yohana Mbatizaji, miaka mia saba na kumi na mbili kabla yeye hajazaliwa, yeye alikuwa "sauti ya mtu aliaye nyikani." Mungu alimwambia Yeremia, "Kabla wewe hata hujaumbwa katika tumbo la mama yako, Mimi nilikujua, na kukutakasa, na kukuweka wakfu kuwa nabii kwa mataifa." Na unapoona manabii wakitokea, hukumu imekaribia.

94 Sasa, "Hukumu huanzia katika Nyumba ya Mungu, na watu wa Mungu." Sasa sisi tuna makosa! Tumefanya makosa. Na mimi naamini kuwa hao walioketi hapa jioni hii, ambao ni Uzao wa Abrahamu na kujulikana halisi tangu asili kwenye Nuru ya Mungu ili ing'ae juu yake; ile Nuru inapoligonga hilo, wao watasimama. Kuna kitu fulani kinachopasa kitukie, hilo ndilo jambo lenyewe! Sasa ninyi mko hapa, hebu tuinamishe vichwa vyetu na kungama makosa yetu.

Rafiki mwenye dhambi, kama wewe umesimama katika hili kundi hapa, ambalo kuna baadhi, uone aibu; lakini baraka kwako sasa, wewe umelipokea hilo, amini hilo kwa moyo wako wote.

Ninyi Wakristo, ninyi wanawake mnaojua, naamini ninyi ni wanawake wazuri. Mungu awabariki. Naamini hilo. Mungu anaweza kuelezea hisia za moyo wangu kwenu. Mimi sitaki kuwa mkatili kwako, dada; mimi ninaye mke, pia, na wawili-wasichana wawili. Nakupenda wewe kama dada yangu.

Na, ndugu, mimi sikutaka kuumiza hisia zako, lakini wakati mwingine kutikiswa kidogo na Neno inakusaidia.

95 Sasa, kama tuna makosa, hebu tuseme kuwa tuna makosa. Na kuna-kuna neema, kwa wingi, kwa ajili yetu jioni hii. "Yeye atakayeungama makosa yake, kuna rehema kwa ajili yake. Yeye atakayeficha dhambi yake, kamwe hatafanikiwa." Dhambi yako ni nini? Kutokuamini kwako. Kama wewe utaficha hilo, useme, "Vema, mimi ni mwema tu kama hao wengine." Wewe unakosea. Na kamwe hutasogea zaidi kuliko pale ulikosogea sasa. Wewe utakaa hivyo hivyo, kamwe hutakwenda mbali zaidi hadi uvuke hicho kizuizi na kufanya hilo kuwa sahihi. Kumbuka, wewe huwezi kufanya hilo; itakupasa utembee juu ya Neno la Mungu.

Na maadam unaishi, siku zote utalikumbuka hili. Siku ndefu zaidi ya zote utakayoishi, utakumbuka jioni hii. Kumbuka, mimi ninakuambia HIVI ASEMA BWANA! Nilikuwa nimeketi msituni alasiri hii, nikiomba, Yeye alinena nami juu ya hili hapa, kasema, "Sema hilo na uliite, nami nitafanya jambo fulani kwa ajili yako." Na ndilo hili hapa.

96 Sasa hebu tuombe. Baba wa Mbinguni, kwa unyenyekevu na kwa uaminifu wamesimama wenye dhambi katika hili kusanyiko sasa hivi. Wao waliinuka kutoka kwenye kiti chao na kutembea kuja juu hapa, ili tu kuungama. Kuna Wakristo ambao wamekuja, wakifanya maungamo yao.

Hapa kuna akina dada wadogo wa thamani ambao ile Nuru iliangaza juu yao, moja kwa moja chini katika moyo wao wao walijua walikuwa wamekosea, wao walijua kuwa Biblia inafundisha hayo mambo, na wao wanakusudia sasa kuondokana na hilo lote.

Hapa kuna ndugu wakiwa wamesimama hapa, ndugu wa thamani, wana wa Mungu aliye hai, ambao, kupitia kanuni ya imani ya dini na hali za uvuguvugu, wametangatanga katika ulimwengu. Wao wanarejea jioni hii, Baba. Wao wanarejea. Wao wako, wao wako hapa.

97 Sasa, Baba, tunatambua kuwa wao waliposimama kwa miguu yao, walivunjika; wanasayansi wote, wao husema kuwa huwezi kwenda juu, unashikiliwa chini. Lakini wao walipoinua juu mikono yao na kutembea njia hii, walithibitisha kuwa kulikuweko na Roho ndani yao ambaye aliweza kufanya uamuzi. Wao wamefanya hilo kwa ajili ya Kristo.

Yesu, hapa kuna Maneno Yako Mwenyewe, na mimi nitayanukuu tu hayo Kwako.

Mimi ninakupa Wewe hawa watu jioni hii, kama mtumishi Wako. Nimefanya tu kama Wewe ulivyoniambia nifanye, leo katika msitu, na hapa kuna lile tu hasa Wewe ulilosema lingetukia. Na kuna mashahidi wa hayo mambo, wakiwa wamesimama hapa. Ili kuthibitisha Wako-Uwepo Wako, Wewe ulikwenda kukatisha kusanyiko, ukiwaambia watu juu ya wao walikuwa akina nani na wapi … walichofanya, na kadhalika, ukijua majina ya watu, na wao walikuwa akina nani na kile wao walichofanya, kile kilicho makosa.

98 Na sasa Wewe ulisema katika Neno Lako, kuwa, "Yeye atakayenikiriMimi mbele za mwanadamu, yeye nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu. Yeye anioneaye aibu mbele za mwanadamu, Mimi nitamwonea yeye aibu mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu." Sasa hawa akina dada na hawa ndugu wamesimama jioni hii katika Uwepo wa washirika wao na wachungaji wao, na wapendwa wao, ili kusema kuwa-kuwa wao hawakuonei aibu Wewe, lakini wanaonea aibu kwa namna wao walivyofanya. Sasa nina hakika, Bwana, kwamba utawasamehe. Wewe uliahidi hilo. Wewe ulisema, "Yeye atakayeungama dhambi zake, anayo rehema." Nao wanaungama hiyo, nao watakuwa na rehema. Na Wewe Ambaye unaweza kuponya wagonjwa, na kusema, "Je, hilo siyo rahisi kusema, 'Dhambi zenu zimesamehewa,' kama lilivyo, 'Chukua kitanda chako na utembee'?"

99 Nawadai hawa. Mimi-mimi namdai kila mmoja wao, Bwana. Nimejaribu kusimama kwa ajili Yako miaka yote hii, na Neno Lako. Nao wamesimama jioni hii kwa ajili Yako, nami nawadai hao. Ninawaondoa kutoka kwenye makucha ya ulimwengu, na nawaleta Kwako, Bwana Yesu. Wao ni tuzo za ushindi za Ujumbe jioni hii, wa Neno la Mungu. Washikilie, Mungu Mwenyenzi, chini ya Nguvu Zako Takatifu. Hebu wao wakue, hebu Nuru ya Mungu imulike katika maisha yao. Hebu hao wanaume na wanawake, Bwana, waanze kukua katika uwezo na nguvu za Roho Mtakatifu. Hebu kitu fulani kitukie ambacho kitabadilisha makanisa yao yote na-na ujirani wote pale waliko. Tujalie hilo, Bwana.

Ninakupa hao, wao ni Wako. Wao-wao ni tuzo za ushindi za mkutano jioni hii, wa lile Neno lililohubiriwa. Nadai uzima wao, katika Jina la Yesu Kristo. Nataka nikutane nao upande ule mwingine, wakati wakiwa wasioweza kupatwa na mauti, wakiwa wamerudi kuwa kijana mwanamume na kijana mwanamke tena, na kuwa kijana na wa kupendeza daima. Wao ni wa Kwako, Baba. Wao ni tuzo za ushindi ambazo Mungu amempa Mwanawe, Kristo Yesu, kwa uwezo wa Uwepo Wake na Neno la Mungu. Wao ni Wako, Baba. Ninakupa hao, katika Jina la Jesu Kristo; na kudai kila uhai, kila uhai uliosimama hapa. Kila ungamo limepokelewa, kila dhambi imesamehewa.

100 Na kila mmoja aliyesimama hapa, mimi-mimi-mimi naomba kwa ajili ya nguvu za Roho Mtakatifu ndani yao, ili kutekeleza, ili kufanya lile ambalo ni sahihi, ili kuwasaidia katika hii saa ya giza wakati ulimwengu umejaa yanayovutia. Na, Ee Mungu, nisaidie kesho jioni, ku-kuleta hilo likiwa safi na wazi kwao, Bwana; na kuondokana na mambo ya kuvutia ya ulimwengu huu, kwamba wao waweze kuwa tayari kukutana na Kristo kwenye ule wakati wa Kuja Kwake. Tujalie hilo, Baba. Tunakuamini Wewe sasa.

101 Na tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu. Kila mmoja wenu mliosimama kwa miguu yenu, mimi siamini mmekuja kwa ajili ya udadisi, kwa sababu mmekuja chini ya kuhubiriwa kwa Injili ambayo ni kali na ngumu, inayoumiza. Lakini unaamini kuwa Yesu alisema kuwa, "Hakuna awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu, na wote Baba alionipa watakuja." Sasa hilo ni Neno la Mungu lililothibitishwa. Yeye alimwambia Abrahamu, Yeye aliahidi na kuapa kwa kiapo, na hapa mmesikia ile Sauti ya Mungu jioni hii na kuja juu ya msingi huo. Inakupasa usamehewe! Na nyote mlikubali hilo na kuamini kuwa Mungu anakusamehe kosa lako, na tangu usiku huu na kuendelea, kwa neema ya Mungu, utaishi kwa ajili Yake maisha yako yote yaliyobakia, na kufanya kila kitu ambacho hii Biblia inafundisha kwa ajili yako kukifanya, na unaamini kuwa Mungu anakupa neema ili ufanye hilo sasa, kwa kukusamehe mambo yako yaliyopita; inua mkono wako, useme, "Mimi naamini hilo kwa moyo wangu wote." Mungu akubariki.

102 Ninyi nyote Wakristo nje kule mnaojivunia hayo, mseme, "Munguatukuzwe kwa ajili ya hayo!" [Kusanyiko linasema, "Mungu atukuzwe kwa ajili ya hayo!"-Mh.] Hebu tuseme hilo tena. [Ndugu Branham na kusanyiko linasema pamoja, ""Mungu atukuzwe kwa ajili ya hayo!"]

Sasa hebu tusimame kwa miguu yetu, kila mmoja. Nataka sauti ya:

Nampenda, nampenda
Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kalvari.

Hebu sote kwa pamoja sasa, kila mmoja aimbe huo tukiwa tumeinua juu mikono yetu. Vema.

Nampenda, nampenda
Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

103 Je, hamjisikii kung'ara hasa? Je, Neno halijakusugua na kukufanya ujisikie vizuri zaidi? Sivyo?

Je, huamini mimi kuwa wa bandia, ndivyo? Je, unaamini mimi kuwa ile Kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina!"-Mh.]

Ninamtazama sasa hivi yule Malaika wa Bwana Ambaye ninamtazama juu ya watu, amezunguka pale pale juu ya hili kundi aliyesimama papa hapa katika umbo la msalaba. Mungu Mbinguni! Picha ile ile mli-…Malaika mnayemwona kwenye picha, yuko hapa hapa sasa juu ya hili kundi la watu, akitembea tu huko na huko, naendelea kuuangalia Huo, tokea mahali hadi mahali. Mimi naamini, hata, kuwa kila ugonjwa uliosimama katika ule umati umeondoka. Na-naamini hilo kwa moyo wangu wote, kuwa kila dhambi imesemehewa.

104 Hebu tushikane tu mkono mmoja kwa mwingine tunapoimba, "Nampenda." "Na …" Useme, "Bwana asifiwe!"

…penda, nampenda
Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Sasa hebu tumsifu tu Yeye, tuseme, "Bwana asifiwe! Asante, Bwana Yesu." Tunakushukuru, Bwana, kwa kuleta watu, na kwa ajili ya Neno Lako. Na ni kali kama upanga wenye makali pande mbili, lakini Hilo linatambua mawazo ya moyo. Hilo linahakikisha. Hilo hutahiri ulimwengu, mwili, huondolea mbali mambo ya kiulimwengu mbali na watu, na kuwafanya wao viumbe vipya katika Kristo. Tunakushukuru Wewe iliyoje, Baba! Tunakusifu Wewe kwa moyo wetu wote. Asante kwa ajili yao, Bwana. Hebu wao wajazwe na Roho! Hebu Roho Mtakatifu awachukue tu hao katika udhibiti Wake, na hebu hapo patokee uamsho wa mtindo wa kale miongoni mwa haya makanisa, Bwana, hiyo itawafagia kwenye jumuia, kila mahali akiwasha moto kwa njia ya nguvu za Mungu. Ututumie pentekoste halisi, Bwana, nguvu halisi ya Roho nyuma katika maisha ya watu. Tujalie hilo, Baba.

Wao ni Wako. Kwa neema ya Mungu, wao ni Wako. Wao ni Uzao wa Abrahamu, kulingana na ile ahadi. Tujalie hilo, Bwana. Wao wanaamini Neno Lako; chochote kilicho kinyume, kama vile hakikuweko. Wao wanaamini Neno kwa sababu wao ni Uzao wa Abrahamu. Wao ni Wako, Baba, Kanisa lililochaguliwa tangu asili ling'ae katika siku ya mwisho. Asante, Baba, kwa ajili yao.

Nampenda…(Inueni mikono yenu sasa katika
kumsifu Yeye.) …Na… (Juu kule roshani, hilo ni
sawa.)
Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza.
Na…

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

*"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7*